Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Tatu – Tarehe 15 Juni, 2006**

(*Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunapoanza kushughulikia shughuli zetu katika Orodha ya leo napenda kuwafahamisha kwamba kwenye *Gallery* ya Spika tunaye mgeni mashuhuru naye si mwingine ni Mheshimiwa Phillip Param ambaye ni Balozi mpya ya Uingereza anayeiwakilisha Uingereza katika nchi yetu. Kulingana na mahusiano mazuri na ya muda mrefu ninafurahi sana kumkaribisha hapa Bungeni na hapa nchini Tanzania, Mheshimiwa Phillip Param. *(Makofi)*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:**

Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2005 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2006/2007.

Taarifa ya Sera za Fedha kwa kipindi cha Mwaka 2005/2006 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa Mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nalazimika kutoa maelezo mafupi mtaona kwenye *Order Paper* ya leo tumepanga maswali manane badala ya kumi. Maelezo ni kama ifuatavyo:-

Swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim swali lililopangwa leo yeye mwenyewe kwa mujibu wa kanuni ndogo ya 4 katika kanuni ya 35 aliamua kuliondoa katika mazingira ambayo hayakutuwezesha kupata kupanga swali lingine kwa sababu kuna utaratibu wa kuyapanga kuwawezesha Waheshimiwa Mawaziri kujiandaa. Swali

lingine ni la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah hili lilikuwa limeulizwa katika Wizara ambayo itagusa pia na mambo ya Bunge. Kwa hiyo, majibu pia yakawa hayapo tayari kwa hiyo tumelipanga sasa lijibiwe na ninamwomba Mheshimiwa Rished Abdallah aiangalie hiyo tarehe yaani tarehe 26 Juni, 2006.Hayo ndiyo maelezo kwa hiyo sasa namwita muuliza swali la kwanza Mheshimiwa George Lubeleje.

## MASWALI

Na. 21

### Ukarabati na Kuongeza Majengo ya Zahanati za Mima na Mbori

**MHE. GEORGE MALIMA LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina mpango wa kuzifanyia ukarabati mkubwa na kuongeza majengo ya zahanati za Mbori na Mima zilizopo Halmashauri ya wilaya ya Mpwapwa ili kuwa na vituo vya afya; na kwa kuwa kujengwa kwa vituo vya afya vya Mima na Mbori kutasaidia sana kutoa huduma za afya katika kata za Mima, Berege, Mbori Mkanana, Matomondo, Kimagai, Godegode, Lumuma na Mbuga:-

(a) Je, Serikali ina maelezo gani kwa wananchi wa Mpwapwa kuhusu utekelezaji wa mpango huo muhimu?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kujengwa kwa Vituo vya Afya vya Mima na Mbori kutasaidia sana kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya wilaya ya Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERILAI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Zahanati ya Mima iko katika kijiji cha Mima katika Kata ya Mima yenye vijiji 6. Zahanati hiyo pia inahudumia wananchi wa Kata za Berege na Mlunduzi. Zahanati ya Mbori iko katika kijiji cha Mbori Kata ya Matomondo yenye vijiji 4. Zahanati hii inahudumia wananchi wa Kata za Kimagai na Godegode. Maeneo yote hayo yana msongamano mkubwa wa watu.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mpwapwa imeshaliona tatizo hili la msongamano wa wagonjwa katika Zahanati hizo hivyo, katika vikao vyake imeamua kulishughulikia. Katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi 9,000,000 ili kufanya usanifu wa majengo na kuandaa gharama za ujenzi ili zahanati hizo ziongezewe majengo na zipandishwe hadhi kuwa vituo vya afya. Serikali

itashughulikia idadi ya watumishi watakaohitajika mara Zahanati hizo zitakapopandishwa hadhi na kuwa Vituo vya Afya.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba iwapo kwa kujengwa kwa Vituo vya Afya vya Mima na Mbori kutasaidia sana kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa. Aidha, huduma kwa wananchi 51,782 na Zahanati ya Mima ikiwa Kituo cha Afya itaweza kutoa huduma kwa wananchi wapatao 53,972. Haya yote yakiwezekana yatapunguza idadi ya wagonjwa wanaopelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa ambao watakuwa na wagonjwa wa kawaida.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, jibu lake ni zuri lakini kwa kuwa bajeti ambayo inatengwa na Halmashauri ya Wilaya hatuwezi kujenga vituo vya afya Mima na Mbori sasa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anakubaliana na mimi kwamba ipo haja ya kuweka fedha maaluma kwa ajili ya kujenga vituo hivyo vya afya ili kupunguza msongamamo wa wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa?

Pili, kwa kuwa darubini ni muhimu sana katika vituo vya afya na zahanati na ili mgonjwa apate tiba sahihi ni lazima achunguzwe ili kuonekana kama ana malaria au ana magonjwa kama ya tumbo. Je, zahanati ambazo hazina darubini Serikali ina mpango gani wa kuimarisha maabara hizo na kuweka darubini kila zahanati ili wagonjwa waweze kupata tiba sahihi baada ya kuchunguzwa na waganga?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninampongeza Naibu Waziri TAMISEMI kwa majibu mazuri aliyoyatoa.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa George Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Vituo vya kutolea huduma vilivyopo hivi sasa kwa maana ya zahanati na vituo vya afya vilijengwa na Serikali yapata miaka 20 sasa na katika kipindi hicho mpaka hivi sasa imeonekana kwamba ipo haja ya kuongeza hivyo vituo na sasa hivi tupo katika maandalizi ya kurudi kwa wananchi, katika muono wetu tumeona kwamba kila kijiji kinastahili kuwa na zahanati na kila kata iwe na kituo cha afya.

Kinachofanyika sasa hivi na Wizara yangu ni kufanya tathmini kwa sababu vituo nilivyovitaja havitakamilika kama hakutakuwa na wafanyakazi kwa hiyo sambamba na ujenzi wa hivyo vituo tunajaribu kuangalia pia *training capacities* kwa kutumia vituo vyetu vya kufundisha, majengo, uwezo pamoja na walimu na vifaa vya kufundishia. Sasa kama mtakavyoona huo utakuwa ni mradi mkubwa kama ule wa MMEM kwa hiyo ninachoomba ni kwamba itabidi tutumie wananchi kujenga hivyo vituo na Serikali inajiandaa kwamba tutasaidia vipi na inapofika hapo sisi Wabunge ndiyo wahamasishaji wakuu twende kwa wananchi wajaribu kutusaidia kujenga hivyo vituo sisi tuweze

kusema kwamba mkijenga Serikali tutajitolea kiasi fulani, kwa hiyo masuala yote pamoja na darubini ni mahitaji ambayo yatakuwa katika mradi huo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 22

**Matunzo ya Watoto Wanaoishi Mitaani, Yatima Walemavu Na Kadhalika**

**MHE. MARIAM S. MFAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Taasisi za Dini, *NGO's* na Watu Binafsi ndiyo wanaojitahidi kutunza baadhi ya Watoto yatima, Walemavu, Waathirika wa UKIMWI na wasio na Makazi Maalumu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujihusisha na matunzo ya Watoto hao?

(b) Je, ni kwa namna gani Serikali inaziunga mkono Taasisi hizo?

(c) Je, ni Taasisi zipi zimeungwa mkono na Serikali katika suala hilo na kwa kiasi gani cha fedha?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Mfaki lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Watoto yatima, watoto wenye ulemavu, waathirika wa UKIWMI na wasio na makazi maalumu ni kati ya watoto walio katika mazingira magumu. Kutokana na ongezeko la idadi ya watoto yatima na walio katika mazingira magumu wizara yangi ilibuni mpango shirikishi jamii wa utambuzi wa huduma za malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto hao.

Mpango huu unatekelezwa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Wadau mbalimbali wa maendeleo. Mpango huu ulianza kutekelezwa tangu mwaka 2000, kwa kushirikiana na shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)* ambapo mpango huo unatekelezwa katika Halmashauri 16 zifuatazo:-

Magu, Makete, Musoma Vijijini, Bagamoyo, Kisarawe, Masasi, Mtwara – Mikindani, Singida Vijijini, Ngara, Kibondo, Manispaa ya Temeke, Manispaa ya Iringa, Jiji la Mwanza, Songea Vijijini na Bunda. Aidha, kwa kushirikiana na Shirika la *Axios Foundation*, *Family Health International*, *Global Fund*, *Africare* na *Pact Tanzania* Mpango huo unatekelezwa katika Halmashauri zingine 16.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka huu 2006 watoto waliotambuliwa katika Halmashauri hizi 32 wameweza kupatiwa huduma zifuatazo:-

- Kuhakikishiwa ulinzi na usalama wao kutoka kwa jamii zinazowazunguka pamoja na Serikali za Vijiji.

- Kujengewa/kukarabatiwa nyumba zao kwa juhudi za Wanajamii.

- Kupewa chakula na wana jamii pamoja na Asasi za hiari.

- .Kwa wanaoishi vijijini kulimiwa mashamba na wanajamii.

- Kulipiwa ada na mahitaji toka Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya dini na Mashirika mengine yasiyo ya kiserikali.

Wizara yangu inakusudia kupanua mpango huu hadi uzifikie Halmashauri zote hapa nchini ili watoto hao waweze kutambuliwa na kuwezeshwa kupata huduma mbalimbali toka kwa jamii na Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inazisajili asasi husika na kuzipa miongozi ya namna ya kutoa huduma zenye viwango vinavyokubalika na jamii. Aidha, Serikali inawashirikisha katika semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kuboresha huduma zinazotolewa na asasi hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikishirikisha na taasisi nyingi ambazo hutoa huduma kwa watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu. Katika miaka miwili iliyopita Serikali imetoa ruzuku kwenye makao 15 ya watoto yatima na wenye shida. Makao hayo ni Nkoaranga, tosamaganga, Mafinga, Ilembula, Bikira Maria, Bujora, Kilangala, Katandala, Musoma, Kwamkono na Kemondo. Serikali itaendelea kutoa ruzuku kwa vituo vingine kulingana na uwezo katika Bajeti ya kila mwaka.Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005 jumla ya shilingi 5,000,000 zilitolewa kama ruzuku kwa wakala wa hiari na mashirika ya dini 11 yanayojishughulisha na malezi ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu, ambapo kwa mwaka 2006/2007 shilingi 300,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kundi hili. Aidha, serikali inaendesha makazi 17 ya wazee wasiojiweza hapa nchini. Jumla ya shilingi 204,000,000 zilitengwa kwa mwaka 2004/2005 kwa ajili ya chakula, malazi na dawa kwa ajili ya makazi hayo 17, mahabusu 5 za watoto, vituo 4 vya ufundi kwa walemavu na kadhalika. Mwaka 2005/2006 jumla ya shilingi 284,000,000 zilitengwa kwa ajili ya shughuli hiyo. Mheshimiwa Mfaki anaweza kupewa orodha ya vituo vilivyofaidika kwa majini kama atahitaji.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika majibu yake ametaja mikoa ambayo imeshasaidiwa kupata msaada kwa ajili ya vituo vya watoto wadogo sasa ningependa labda nijue mkoa wa Dodoma ni kwa nini haujaingizwa katika msaada huo wakati na wenyewe una watoto wadogo.Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Mfaki, kama ifuatavyo:

Kama nilivyozungumza katika majibu yangu ya msingi kwenye swali lake la msingi kwenye swali lake la msingi ni kwamba vituo ambavyo vimepata msaada na wilaya ambazo zilikuwa zimetajwa ni kwa zile ambazo pesa zilikuwepo sasa kwa sababu tunaendelea na mikoa mingine kama nilivyosema awali pesa itakapokuwa inapatikana tutaendelea ndiyo maana nikasema mikoa mingine Serikali inafanya jitihada ya kuweza kuifikia.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Naibu Waziri amezungumzia suala zima la kutambua watoto yatima, walemavu na waathirika wa UKIMWI lakini pia ongezeko la watoto wasio na makazi maalumu limekuwa kubwa hivi Serikali ina mpango au utaratibu gani wa kupunguza watoto wa aina hii ambao mara nyingi huwa wanapatikana katika ndoa zisizo rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, matatizo ya watoto ambao wamejaa mitaani kutokana na kutokuwa na mahali pa kukaa hasa inatokana na jamii yetu wenyewe na Serikali ina mkakati wa kuleta sera ya familia ya kuhamasisha wananchi wachukue jukumu lao la kulea watoto, jamii ina jukumu kubwa la kulea watoto ikumbukwe kwamba hali haikuwepo zamani kwa hiyo bado kila kitu kitarudi kwetu sisi jamii na Mheshimiwa Mbunge ni vema kama ukihamasisha jamii yako kuhakikisha kwamba watoto ambao hawana malezi bora wanapata malezi. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 23

**Ugonjwa wa UKIMWI**

**MHE. ELIETTA N. SWITI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inajitahidi kutoa matangazo mengi katika juhudi za kupunguza kasi ya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI bila mafanikio yoyote:-

Je, Serikali inaweza kutoa maelezo sasa kwa wagonjwa wa UKIMWI mara wanapopima na kugundulika waambiwe ili wasiendelee kuambukiza wenzao kwa kuamini wao ni wazima?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kutoa maelezo mafupi kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Elietta Switi, Mbunge wa Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Kulingana na Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya mwaka 2001 sura ya 3 kipengele kinachohusu kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari, mambo yafuatayo yanazingatiwa:-

1. Ushauri nasaha kabla na baada ya kupimwa utafanywa ili kumwezesha mtu kupewa matokeo ya vipimo vyake, na kama ni mdogo matokeo ya vipimo hutolewa kwa wazazi wake. Lengo kuu la kutoa ushauri nasaha ni kuwawezesha wateja kuzingatia na kuchukua tahadhari ili wasiambukizwe kama hawajaambukizwa; kadhalika wale ambao wameambukizwa tayari, wapate ushauri ili wakubaliane na hali zao, pamoja na kuchukua tahadhari ili wasiambukizwe tena au kuambukiza wengine virusi vya UKIMWI.

2. Kwa upimaji ambao anayepima hatambuliki *(un-linked HIV testing*) kwa mfano wakati wa utafiti, ushauri nasaha wa kabla na baada ya kupima hautahitajika. Hata hivyo watu wanaojitolea kutoa damu ambao watapenda kujua matokeo ya vipimo vyao, taratibu zitawekwa za kufuatilia vipima vya virusi vya UKIMWI kwa hiari na kupata ushauri nasaha kabla na baada ya upimaji.

Kuhusu kutoa matokeo ya vipimo kwa mtu mwingine ambaye si yule aliyepima, sera imeeleza wazi kwamba ridhaa ya kutoa taarifa baada ya ushauri nasaha wa kutosha itaombwa kwa mhusika (anayepimwa) kabla upimaji haujafanywa. Kwa wagonjwa waliolazwa hospitalini, au wagonjwa waliopoteza fahamu na wale wanaoonekana kwamba hawana akili timamu, ushauri nasaha utamhusisha ndugu wa karibu zaidi kutoa idhini kabla ya kuanza uchunguzi na matibabu.

Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Elietta Switi Mbunge, Viti Maalumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba juhudi za Serikali za kutoa matangazo dhidi ya kupunguza kasi ya maambukizo ya ugonjwa wa UKIMWI hazijakuwa na mafanikio yoyote. Wananchi wengi sasa wanauelewa ugonjwa wa UKIMWI pamoja na dalili zake na hii imedhihirishwa kwa wengi kujitokeza kupima afya zao kwa hiari. Watoa huduma wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamiii wanawaelekeza watu wanaopimwa na kugundulika kwamba wameambukizwa virusi vya UKIMWI kama ifuatavyo:-

(a) Kila mtu atakayetaka au kushauriwa kupima virusi vya UKIMWI hupewa majibu yake baada ya kupata ushauri nasaha. Ushauri huo hutolewa kabla na baada ya kupima ili kumwezesha kupokea matokeo ya vipimo vyake kwa urahisi.

(b)Kama atakutwa ameambukizwa anapewa ushauri nasaha wa kumwezesha kuyakubali matokeo hayo na anashauriwa jinsi ya kujikinga asiambukizwe au kuambukiza watu wengine.

(c)Anaelekezwa kuwa tayari kupokea dawa na ategemee nini pindi matibabu yatakapoanzishwa.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na pia namshukuru sana Waziri wa Afya kwa majibu mazuri lakini napenda kuongeza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kutokana na imani za uchawi au woga wengi wa wagonjwa hawaendi kupima kwa wakati muafaka na kwa kujipeleka wenyewe hospitali, wakati mwingine huambiwa majibu wakati wameshakuwa hoi au baada ya kufa kwao ndiyo jamii zao wanaambiwa.

Je, Serikali ina mpango gani kutusaidia katika hili? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Elietta Switi, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema awali suala la UKIMWI kuna mambo mengi ambayo yanazungumziwa yanayohusiana na kutokuelewa lakini kama ninavyosema Serikali inachukua jitihada za kuweza kuwaelimisha wananchi ili kuzingatia yale wataalamu wanayoeleza kuhusu suala zima la UKIMWI kwa wale ambao wanashindwa kwenda kupima au wanakuta kwamba wanapimwa wakati hali zao zimekuwa mbaya sana na kupewa majibu sisi bado tunaendelea kusisitiza kwamba suala la kupewa majibu inatakiwa uzingatie kumpa yule ndugu wa karibu kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kama nilivyosema kwamba kama mgonjwa yupo taabani au amepoteza fahamu basi ndugu wa karibu wanatakiwa waelekezwe.

Kwa hiyo, bado naendelea kusisitiza kwamba suala la kupewa majibu na suala la kupima afya ni suala la hiari na majibu yanatakiwa yapewe kwa yule ambaye anakubali kupokea au ndugu yake ambaye ameandaliwa kupokea majibu hayo.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, nakumbuka Jerry Rawlings (Rais wa zamani wa Ghana) alipofika hapa Tanzania, Dodoma alisema anayeambukiza UKIMWI kwa makusudi ni sawasawa na mtu aliyeuwa kwa makusudi.

Je, kwa wale wagonjwa wa UKIMWI ambao wanafahamu na wamepewa *councelling* na wanajijua lakini kwa makusudi kabisa wanaambukiza UKIMWI maana yake wanaua, kuna taratibu gani ya kuwathibiti? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna watu ambao wanajifahamu kabisa kwamba wao wameambukizwa na wana matatizo ya UKIMWI lakini wanasambaza kwa makusudi kabisa wakati wanajua hali za afya zao.

Mheshimiwa Spika, hii ni kweli kabisa kwamba ni kosa lakini Wizara inaanda utaratibu ili kuweza kurekebisha katika kuleta sheria katika Bunge lako Tukufu ili hawa watu waweze kubanwa kwa sasa hivi hakuna sheria ambayo inaweza kumbana mtu hata kama anafahamika na kuweza kumshitaki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kupitia Bunge lako Tukufu Wizara ya Afya bado inafanya maandalizi baadaye itakapokuja hapa nitawaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane ili tuweze kuzuia kusambaa kwa ugonjwa huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Elisa Mollel kwa swali linalofuata nimepokea karatasi la malalamiko kuhusu mwanga mkali sana wa taa katika baadhi ya sehemu walizokaa Waheshimiwa Wabunge.

Ningeomba mambo mawili, moja kwa sasa hivi wanaruhusiwa kuhamia kiti chenye ahueni watakachokiona kwa sasa hivi lakini baada ya hapo naomba Katibu wetu wa Bunge apate orodha ili marekebisho ya kiufundi yafanywe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 24

**Usambazaji wa Umeme Vijijini**

**MHE. ELISA D. MOLLEL** aliuliza:-

Kwa kuwa, umeme ni nyenzo muhimu katika kuchokea maendeleo ya wananchi vijijini, na kwa kuwa Serikali imedhamiria kusambaza umeme Vijijini. Je, ni lini Serikali itawapatia umeme Wananchi wa Vijiji vya Oldonyosambu, Oldonyawas, Lemanyata, Likindinga, Olasiti, Midawe na Mirongoine katika Jimbo la Arumeru Magharibi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo.

Serikali pamoja na Shirika la Umeme itaendelea kusambaza umeme katika vijiji mbalimbali nchini kulingana na uwezo wa kifedha na bajeti iliyopo. Baadhi ya vijiji alivyotaja Mheshimiwa Mbunge vimeanza kupatiwa umeme kwa bajeti ya Shirika kwa mwaka huu wa fedha wa 2005/2006. Sehemu ya kijiji cha Midawe imeshapata umeme kwa gharama ya shilingi 13,161,350.59 na mradi huu bado unaendelea kutekelezwa. Kwa upande wa kijiji cha Olasiti, jumla ya shilingi 23,884,626.00 zilitumika kupeleka umeme sehemu ya kijiji hiki na sehemu ya kijiji iliyobaki itapatiwa umeme mara fedha zitakapopatikana. Aidha, chini ya mradi wa Benki ya Dunia *ERT* ambao sasa hivi unafanyiwa upembuzi yakinifu, vijiji vilivyobaki vitapatiwa umeme. Makadirio ya gharama za kuvipatia umeme vijiji hivyo yameishafanywa na ni kama ifuatavyo:-

(a) Oldonyasambu, Oldonyawas na Lemanyata, gharama ni shilingi 99,759,900.00;

(b) Likindiga, gharama ni shilingi 36,500,000.00; na

(c) Mirongoine pamoja na vijiji vya Mbuguni, Laswaki, Terrati, Oiborkishu na Haramatak, Lorkonerei ambavyo kwa pamoja vitakuwa na njia ya umeme yenye urefu wa kilomita 49, gharama yake ni shilingi 754,372,664.00.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani watu wa Arumeru watashangaa majina ya Vijiji vyao.

Ningeomba kuuliza kwa kuwa Bunge hili limepitisha mfuko wa umeme vijijini, nadhani ni mwaka jana. Ni lini mfuko huo utaanza kazi ili vijiji vyote vinavyostahili kupata umeme vianze kupata umeme kwa ajili ya mfuko huo?

Swali la pili, kwa kuwa kijiji kilichotajwa cha Oldonyosambu kinapakana na kijiji cha Engikare ambacho kiko katika Jimbo langu. Je, ni lini umeme utapelekwa katika kijiji hicho katika mpaka wa Longido na gharama ni kiasi gani? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sehemu ya pili ya swali la nyongeza inayotajwa ni kijiji kipya kabisa pamoja na kudai gharama nadhani ni vizuri lingeulizwa kama swali pekee. Ningeomba ujibu swali la kwanza la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mfuko wa usambazaji umeme vijijini unafanyiwa kazi na Bodi inazinduliwa hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba harakati ya Serikali kuhakikisha kwamba vijiji vyote hapa nchini vinapatiwa umeme inafanyiwa kazi. Nilivyoeleza katika swali la msingi pale fedha zitakapopatikana vijiji hivyo vitapatiwa umeme.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali ndogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa vijiji vingine vilishapitishwa kwamba vitapata umeme kama kijiji cha Bukene na kijiji cha Ndala katika Wilaya ya Nzega; na kwa kuwa ni busara kumaliza ahadi ya vijiji vilivyopitishwa kabla ya kuanza kazi nyingine. Je, kijiji cha Bukene na cha Ndala vitapata umeme lini ili viweze kupata maendeleo kwa wananchi wake?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu kwamba pengine ni bora kumaliza maeneo ambayo yaliahidiwa zamani kabla kuanza maeneo mapya.

Mheshimiwa Spika,m naomba kumwomba Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu afanye subira. Tuna imani kwamba katika bajeti ya mwaka huu kama mambo yote yatakwenda sawasawa kama tunavyotarajia baadhi ya maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba hayajapatiwa umeme na yaliahidiwa uenda yakatizamwa kwa sura mpya na uenda yakapata umeme. Kwa hiyo, nadhani tufanye subira, tusubiri bajeti ya Wizara itakapofika.

**MHE. VITA RASHID KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika Halmashauri ya Namtumbo Kaimu Mkurugenzi wetu alifariki kwa kuungua moto akiwa katika harakati za kupata mafuta ya *generator* ya ofisi kufanya kazi usiku. Sababu ya msingi ni kukosekana kwa umeme. Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wananchi wa Namtumbo watapatiwa umeme katika kipindi hiki cha miaka mitano ya Awamu ya Nne? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi katika Ilani yake ya Uchaguzi imeahidi Serikali itakayoundwa na ambayo sasa imeishaundwa kufikisha umeme katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Katika maeneo ambayo yametajwa ni maeneo ya Mkoa wa Ruvuma.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka katika Mkoa na Ruvuma na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwamba Serikali ina mipango mahsusi ya kuhakikisha kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano, basi Mkoa wa Ruvuma unafikishiwa umeme wa gridi na kazi hiyo kwa kweli imeishaanza kwa maana ya ujenzi wa kituo cha kupoozea umeme cha Makambako ambacho nilikitembelea wiki iliyopita.

Naomba nitoe matumaini kwamba katika kipindi cha miaka mitano Mwenyezi Mungu akijalia tutaweza kufikisha umeme katika Mkoa huo wa Ruvuma na hivyo katika Wilaya hiyo aliyoisema.

Na. 25

**Utafiti na Uchimbaji wa Madini**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kumekuwepo harakati za utafiti na uchimbaji wa madini (*drilling*) kwa zaidi ya miaka sita (6) huko Lukoma kati ya Mwese na Mwambao wa Ziwa Tanganyika:-

(a) Je, ni nini matokeo ya utafiti huo na kwa sababu gani umechukua muda mrefu?

(b) Kwa kuwa, Makampuni ya *Geo-Search, Drill Corp, Stanley* na *Tan Drill* kwa nyakati mbalimbali yamekuwa yakifanya kazi Lukoma. Je, nini mahusiano ya Kampuni hizo na matokeo ya utafiti wa kila kampuni?

(c) Je, utafiti huo wa muda mrefu umelinufaisha Taifa kwa kiasi gani au ni hasara kiasi gani ambayo Taifa limepata kutokana na kuchukuliwa mawe yanayochimbwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya jumla kuhusu swali hili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya utafutaji wa madini hupitia hatua mbalimbali kwa kuhusisha nyanja za utafiti wa kijiolojia, kijiokemia na kijiofizikia. Matokeo ya kazi hizo ni muhimu ili kujua aina na ukubwa wa mashapo ya madini yanayopatikana katika maeneo husika kabla ya hatua za uendelezaji mgodi kuchukuliwa.

Chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 1998, leseni za utafutaji wa madini, yaani *Prospecting Licence*, huweza kuendelea kuwa hai hadi muda wa miaka saba. Hata hivyo, kazi ya utafutaji madini inaweza kuchukua muda mrefu zaidi kutegemea mazingira ya kijiolojia yaani (upatikanaji wa madini ya kutosha kufungua mgodi) na mazingira ya kiuchumi, hususan mwenendo wa soko la madini yanayotafutwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya jumla, sasa napenda kujibu swali la msingi la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Nyati Mining Company Limited* ya Australia imekuwa ikifanya utafutaji wa madini katika eneo la Lukoma tangu mwaka 2000 ilipopewa leseni ya utafutaji mkubwa wa madini, yaani *Prospecting Licence*. Kimsingi, utafiti huo haujawezesha kugunduliwa kwa mashapo ya kutosha kufungua mgodi, licha ya kugunduliwa kwa madini ya kundi la *Platinum* (*Platinum Group of Elements*). Utafiti huo umechukua muda mrefu kwa sababu ya kutopatikana madini ya kutosha kufungua mgodi kama ilivyoelezwa hapo juu.

(b)Mheshimiwa Spika, Kampuni za *Geo-Research, Drill Corp, Stanley* na *Tan Drill* zilikodiwa na mmiliki wa leseni, yaani *Nyati Mining Company Limited*, ili kufanya uchorongaji wa miamba kama moja ya njia za utafutaji wa madini kwenye eneo la Lukoma.

(c)Shughuli za utafutaji madini zina manufaa mbalimbali kwa Taifa. Manufaa ya msingi ni upatikanaji wa taarifa za kina za utafiti wa madini. Taarifa hizo ni muhimu kwa Taifa ili kubainisha utajiri wa madini uliopo na mifumo ya kijiolojia ya sehemu mbalimbali za nchi na pia kuwavutia wawekezaji katika sekta ya madini, wa nje na ndani ya nchi, ili wawekeze kwenye sekta ya madini nchini. Aidha, kazi za

utafutaji madini huchangia kutoa ajira, kuongeza biashara za bidhaa za ndani na kuboresha miundombinu katika maeneo ambayo shughuli hizo hufanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa Serikali haipati hasara kwa mawe yanayochukuliwa kama sampuli kwa ajili ya utafiti wa kimaabara. Aidha, upelekaji wa sampuli za kijiolojia kwenye maabara ni sehemu muhimu ya utafiti wa madini.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

(a) Ni kwamba tafiti ni lazima zifike katika maabara. Katika miaka ya 70 maabara na Kituo cha Utafiti wa Madini hapa Dodoma kilikuwa kinaongoza katika Afrika ya Mashariki na ya Kati. Sasa kimesaidiwa na kuboreshwa kwa kiasi gani ili hizi tafiti zote ziweze kufanyika nchini badala ya kupeleka sampuli zetu nje ya nchi?

(b) Je, Serikali inawakilishwa kwa kiwango gani katika maeneo ambayo tafiti zinafanywa au ni shamba lisilokuwa na mwenyewe basi wameachiwa makampuni wafanye wanavyotaka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ningependa kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba utafiti ambao unafanyika unasimamiwa kikamilifu na Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini. Sampuli zote ambazo zinachukuliwa huwa zinatathminiwa na Wizara yetu kwa kupitia *G.S.T.* na huwa inahakikishia kwamba tathmini zote tunazofikishiwa ni sahihi ili kuhakikisha kwamba mashapo ambayo tunaelezwa yapo na yapo kweli.

Ningependa kuwahakikisha kwamba Serikali inafanya kila jambo kuhakikisha kwamba utafiti na maabara ambao upo hapa Dodoma uweze kufanya kazi kwa kikamilifu na pale ambapo tutafikia uwezo wa kuhakikisha kwamba utafiti wote ufanyike hapa nchini tutajitahidi. Lakini lazima tufahamu kwamba kuna aina mbalimbali za utafiti ambazo kutokana na jiolojia ya sehemu yenyewe lazima zipelekwe nje. Lakini watu wetu hapa huwa wanafanya tathmini na kuhakikisha kwamba haipelekwe nje kiholela.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mimi ningependa kufahamu kama Serikali inatambua kuwapo kwa watafiti wenyeji ambao kwa miaka mingi wamefanya utafiti kwa gharama kubwa na kugundua maeneo mengine sana ya machimbo. Lakini yanapozaa matunda basi hatua zinachukuliwa za kuwaondoa pale kwa kutumia nguvu ya Polisi na hatimaye wanabakia kuwa wakimbizi wa ndani na maeneo hayo hupewa wachimbaji wakubwa. Wakati Sheria ya Madini imeainisha kwamba kutakuwa na maeneo ya wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa. Sasa yale maeneo ya wachimbaji wadogo ambayo yamechukuliwa yatarudishwa lini kwa wenyewe? Hilo ndilo swali langu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chacha Wangwe nasikitika hilo ni swali jipya kabisa. Swali lililo mbele yetu linahusu Utafiti wa Madini, unalouliza ni Sera ya Upangaji wa Watu Vijijini maeneo yaliyo na madini. Kwa hiyo, tuna muda mpaka tarehe 15 Agosti, 2006 unaweza ukaliuliza moja kwa moja kwa maandishi. Ahsante.

Na. 26

**Vitambulisho vya Uraia**

**MHE. FELISTER A. BURA** atauliza:-

Kwa kuwa, tangu tupate Uhuru Watanzania hawajawahi kuwa na vitambulisho vya uraia zaidi ya hati ya kusafiria na kadi za vyama vyao vya siasa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa raia wake kukosa vitambulisho, wageni wasio raia wanafaidi rasilimali ya nchi yetu isivyo haki yao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa vitambulisho kwa raia wake na kwa kipindi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa vitambulisho vya uraia hapa nchini. Kwa kutambua umuhimu huo Serikali imetenga shs. 3bn/= katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007 kwa ajili ya maandalizi ya kutekeleza mradi huu.

Hivi sasa upembuzi yakinifu kuhusu mradi huu umekamilika na maandalizi yanafanyika ya kutangaza tenda ili kupata kampuni yenye ujuzi wa kutekeleza kazi hii. Iwapo mambo yote yatakwenda sawa vitambulisho vitaanza kutolewa mwaka wa fedha 2007/2008.

Wakati maandalizi yanafanyika ya kutekeleza mradi huu, napenda kutoa wito kwa viongozi wa Serikali za vijiji na mitaa pote nchini kuharakisha zoezi la kuwaandikisha watu wasio raia wanaoishi katika maeneo yao. Zoezi hili limeanza kwenye Mikoa ya mipakani.

Mheshimiwa Spika, zoezi hili ni muhimu lifanyike kwa makini sana ili wakati ukifika wa kutoa vitambulisho hivyo vya uraia visiangukie mikononi mwa wageni.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi walio wengi wanaishi vijijini na wako mbali na Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa yao. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba wakati utakapofika wa kutoa vitambulisho hivyo wananchi hao hawatapata usumbufu wa kufuata vitambulisho katika Makao Makuu ya Wilaya au katika Mikoa yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mpango mzima wa kutoa vitambulisho utahusu pia ufunguaji wa Vituo Maalum vya kuhakiki, kuorodhesha pamoja na kutambua raia wa nchi yetu kuanzia Makao Makuu ya Uhamiaji hadi Mikoani.

Kwa hiyo, napenda kulihakikishia Taifa na Mheshimiwa Mbunge kwamba kutakuwa na Vituo Maalum karibu na sehemu za wakazi ambao ni Watanzania milioni 17 wa kwanza watakaorodheshwa na zoezi hili litakwenda bila usumbufu kwa wananchi.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa uraia uko tofauti tofauti kama vile wa kuzaliwa, wa tajinisi, ule wa urithi na pengine wakati fulani mtoto anapokuwa mdogo anakuwa na uraia wa aina mbili. Serikali imejiandaa vipi kutoa vitambulisho tofauti tofauti ili kuyatambua makundi hayo na ukitilia maanani kwamba mpaka wakati huu Uhamiaji hawajafanya utafiti wa kutosha wa kujua makundi ya raia hawa. *(Makofi)*

Je, Serikali imejiandaa vipi hasa kama vile nchi nyingine duniani zinavyofanya kuyatambua makundi na kutoa vitambulisho tofauti tafouti kwa maana ya rangi na umuhimu wake kwa ajili ya faida ya Taifa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba uko uraia wa kuzaliwa, uko wa kuandikishwa na uko wa kurithi. Lakini ukishakuwa raia katika aina zote hizo basi ni raia, hakuna raia *grade one*, *grade two* na *grade three.* Kwa hiyo, vitambulisho hivi vitakapotoka kila raia ambaye ni Mtanzania atakuwa na haki ya kupata kitambulisho. Isipokuwa tutakuwa na vitambulisho vingine kwa ajili ya wageni. Kwa hiyo, tutakuwa na vitambulisho vya aina mbili tu vya raia ambao ni raia wa aina zote na vile vya wageni halali ambao wapo nchini nao vilevile tutawapa vitambulisho.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naona bado tuna muda. Kwa hiyo, swali la nyongeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Sheria ya Vitambulisho vya Uraia imepitishwa miaka 19 iliyopita tokea mwaka 1987 na sababu moja kubwa ya Serikali kuchelewa kutekeleza mradi huu ni mradi mkubwa. Kwa kuwa *information* zinazotakiwa katika vitambulisho zinahusisha Wizara nyingi. Je, Serikali haioni ni busara kukusanya Idara zote ambazo zitatakiwa takwimu zake au taarifa zake ziwekwe katika vitambulisho ili kuanzishwe Mfuko mmoja mkubwa wa kuweza kutengeneza

vitambulisho kwa haraka badala ya kuendelea kuweka fedha kidogo kama hivi wakati Sheria imeishachukua muda wa miaka 19 sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli baada ya miaka yote hiyo kususua Wizara ya Mambo ya Ndani inashirikisha vyombo mbalimbali katika kuratibu, kuorodhesha na kuthibitisha uraia wa wananchi wanaolengwa kufanyia kazi hiyo. Sasa hivi katika utafiti uliofanywa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimehusika zaidi katika kulishughulikia suala hili na vyombo na Wizara zote zinazohusika na masuala mazima ya uraia ikiwemo hata Wizara ya Usalama wa Uraia vinahusishwa katika jambo hili ili kuwezesha Taifa kupata takwimu kamili na sasa hivi tumepania kulikamilisha katika kipindi cha miaka miwili ijayo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona na ninashukuru kwa majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa sasa hivi vitambulisho vya makazi hakuna na hata vile vipande vya kodi ambavyo wananchi walikuwa wanavitumia kama vitambulisho hakuna kwa sababu kodi zimefutwa. Je, Serikali itahalalisha vitambulisho vilivyotolewa na Tume ya Uchaguzi ya Taifa vianze kutumika kwa wananchi wa vijijini kwenye shughuli mbalimbali kama vile posa na kadhalika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kiini cha tatizo kubwa la utengenezaji wa vitambulisho vya Kitaifa ni kuhusu utambuzi wa hasa nani ni raia wa Tanzania. Sehemu ya sensa ni mojawapo, lakini Wizara inakwenda zaidi ya sensa. Inaangalia kumbukumbu za uzawa yaani watu waliozaliwa, ndoa, talaka pamoja na vifo. Sehemu zote hizo zina uthibitisho au zina dalili ya kuonyesha Mtanzania ni nani, lakini tunakwenda pia zaidi ya hapo. Kuna kuangalia shule watu walizosoma, wafanyakazi sehemu za kazi na *affidavits* yaani hati ambazo zinajaribu kuthibitisha huyu ni Mtanzania wakati anapoomba Pasipoti kwa mfano au anapoomba uraia wa nchi hii. Maeneo yote hayo yanaangaliwa ili kujua Mtanzania hasa ni nani.

Kwa hiyo, wale waliojiandikisha wakati wa sensa ni dalili mojawapo au ni kigezo kimoja ambacho Serikali itakiangalia wakati ikiangalia ushahidi mwingine wa kuthibitisha iwapo wale watu wote waliojiandikisha wakati wa sensa kwa kweli ni Watanzania wanaostahili kupata vitambulisho vya Kitaifa.

Na. 27

**Jukumu la Kuhifadhi Wakimbizi**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkoa wa Kigoma umepewa jukumu kubwa, zito na hatari la kuwahifadhi wakimbizi toka nchi jirani.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapa fidia wananchi wa Mkoa wa Kigoma kutokana na madhara ya kuharibiwa mazingira, usalama mdogo kutokana na ujambazi na kupoteza maisha kwa baadhi ya wananchi kunakosababishwa na hao wakimbizi?

(b) Je, kwa nini jukumu hilo gumu umepewa Mkoa wa Kigoma na Kagera tu?

(c) Je, Serikali kwa kushirikiana na Mataifa ya Kimataifa kama vile *UNHCR* ina mkakati gani endelevu wa kusaidia maeneo yaliyoharibiwa kwa ujio wa wakimbizi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa Mikoa inayohifadhi wakimbizi kutoka nchi jirani za Burundi na *Congo (DRC).* Ni kweli pia wakimbizi hao wamesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na kuhatarisha usalama wa raia wanaishi maeneo yaliyo jirani na makambi ya wakimbizi.

Kwa kuwa madhara ya wakimbizi yamewagusa wananchi wote wanaoishi katika Mikoa inayohifadhi wakimbizi na nchi nzima kwa namna moja au nyingine, Serikali kwa sasa haina mpango wa kumlipa fidia mwananchi mmoja mmoja.

Hata hivyo, kwa mujibu wa sera ya wakimbizi, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa imeanza miradi maalum ya kijamii katika Mikoa inayohifadhi wakimbizi kwa ajili ya kukabiliana na athari za wakimbizi ikiwa ni pamoja na miradi ya kukarabati shule, Hospitali, Zahanati, barabara, upandaji miti na kadhalika. Hivi sasa kupitia ufadhili wa Serikali ya Denmark zimetengwa Shs. 9bn. kwa ajili hii ya Mkoa wa Kigoma pamoja Wilaya ya Ngara.

Aidha, ili kukabiliana na wimbi la ujambazi, Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa hasa Jumuiya za Ulaya itaendelea kuimarisha ulinzi kwa kuweka vikosi maalum katika maeneo yenye wakimbizi ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Kigoma na Kagera inahifadhi wakimbizi toka nchini za jirani zenye migogoro ya kisiasa hasa Burundi na *Congo (DRC)* kwa kuwa inapakana na nchi hizo. Sheria ya Kimataifa zinaelekeza makambi ya wakimbizi yawekwe jirani na wanakotoka ili iwe rahisi kuwarejesha makwao pindi hali inaporuhusu.

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili utapatikana baada ya wakimbizi wote kurejea makwao. Hivi sasa Serikali kwa kushirikiana na *UNHCR* inaendesha zoezi la kuwarejesha makwao wakimbizi wa Burundi na *Congo (DRC).*

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, aliwahi kubaini na kupendekeza yatengewe maeneo ndani ya nchi walizotoka ili wakae huko je, Serikali inaweza kutekeleza sasa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Serikali iliyopita tamko lilitolewa kwamba ni vyema wakimbizi hao wakatengewa maeneo maalum ndani ya nchi wanazotoka ili kupunguza mzigo wa kubeba wakimbizi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya zoezi hili halikuwa limefanikiwa kwa sababu uamuzi wa kuwahamisha wakimbizi kwenda kwenye eneo lililotengwa ndani ya nchi wanazotoka kwanza kidogo linapingana na sheria za Geneva zinazotawala haki za wakimbizi ambazo zinataka wakimbizi waende kwenye nchi ambayo wanaridhia kwenda kuishi. Lakini pili, tulipata matatizo kidogo kwa sababu suala hili la kuhamisha wakimbizi kwenda nchi jirani linahitaji ushirikiano wa nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania hatukupata ushirikiano huo.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema kwenye swali la msingi tunadhani ufumbuzi wa kudumu ni amani na utulivu katika nchi wanazotoka wakimbizi hao mara inapopatikana kama sasa hivi hali ilivyo Burundi na Kongo wataondolewa ili warudi makwao. Kwa hiyo, ningependa kumalizia kwa kusema tunaziomba sana nchi zinazopakana na sisi zitekeleze suluhu ili tuwarudishe wakimbizi na tuondokane na mzigo wa wakimbizi tunaoubeba.

Na. 28

**Tume ya Pamoja Kati ya Tanzania na Msumbiji**

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania na Msumbiji ni nchi jirani ambazo watu wake ni wamoja walioshirikiana vizuri wakati wa vita vya ukombozi wa Msumbiji vilivyoung'oa utawala wa Kireno mwaka 1975; na kwa kuwa, baada ya uhuru wa Msumbiji iliundwa Tume ya Pamoja kati ya Tanzania na Msumbiji ili kukuza ushirikiano wa nchi hizo mbili:-

(a) Je, Tume hiyo imefanya vikao vingapi tangu ilipoundwa na vilifanyika nchi gani?

(b) Je, ni mafanikio gani yamepatikana tangu kuundwa kwa Tume hiyo?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha uhusiano mzuri uliopo kati ya nchi hizo mbili hasa katika nyanja za siasa na uchumi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. Mstaafu George Huruma Mkuchika, Mbunge wa Jimbo la Newala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Tanzania na Msumbiji ziliunda Tume ya Pamoja ya Ushirikiano mwaka 1975, mara tu baada ya nchi ya Msumbiji kupata uhuru wake.

(i) Maeneo ya ushirikiano yaliyoainishwa katika Tume hii ni pamoja na biashara, elimu na utamaduni, usalama wa anga, uhamiaji, mawasiliano na uchukuzi, usalama wa raia, utalii na uwekezaji.

(ii) Mpaka sasa Tume hiyo imefanya vikao vitatu. Kikao cha kwanza kilifanyika Dar es Salaam mwaka 1975, kikao cha pili kilifanyika Maputo mwaka 1976 na kikao cha tatu kilifanyika tena Dar es Salaam 1992. *(Makofi)*

(b)Mheshimiwa Spika, tangu kuundwa kwa Tume ya pamoja kati ya Tanzania na Msumbiji, mafanikio ambayo yamepatikana ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kuimarika kwa undugu wa wananchi wa nchi zote mbili;

(ii) Kupitia mikataba mbalimbali ya kisekta, tumeweza kuimarisha ushirikiano wetu katika Sekta ya Biashara, Ulinzi na Elimu;

(iii) Tumeweza kuwa na msimamo wa pamoja katika masuala mbalimbali ya Kikanda na ya Kimataifa; mfano katika Umoja wa Mataifa na katika Jumuiya ya *SADC.*

(c) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kuimarisha uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na Msumbiji ni pamoja na:-

(i) Kuendeleza ushirikiano mzuri uliopo;

(ii) Tumeanza kufanya maandalizi kwa ajili ya kikao cha nne kinachotarajiwa kufanyika mjini Maputo Msumbiji mnamo Septema 2006;

(iii) Kupitia maeneo ya ushirikiano yaliyopo ili kuainisha maeneo machache yanayotekelezeka na yenye tija zaidi kwa wananchi;

(iv) Kuendeleza miundombinu ya pamoja inayolenga kuimarisha uhusiano wa kiuchumi kati ya nchi hizi mbili. Uwekaji wa jiwe la msingi wa Daraja la Umoja ni moja ya hatua muhimu;

(v) Tanzania na Msumbiji zipo katika hatua ya mwisho ya kukamilisha mkataba wa kuondoa matumizi ya Visa kwa wananchi wake. Kukamilisha kwa mkataba huu kutaimarisha uhusiano wa nchi hizi mbili katika nyanja mbalimbali hasa katika biashara.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ya swali langu. Kama ilivyoonyeshwa ni zaidi ya miaka kumi Tume ilikuwa haijakutana na nimefarijika kumsikia Mheshimiwa Waziri kwamba maandalizi yanafanyika ili tume ipate kukutana tena.

Mheshimiwa Spika, nina swali dogo tu la nyongeza. Je, Mheshimiwa Waziri kwa ari ile ile uliyonayo ya kutaka kuimarisha uhusiano wetu wa Tanzania na Msumbiji unaweza kuniahadi au kutuahidi Watanzania kwamba kwa sababu Wizara ya Mambo ya nje ndiyo kinara wa mambo ya mahusiano kwamba zile Wizara zilizotajwa katika jibu lako kwamba utakutana nao na wao nao waanze kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya kama ulivyoanza wewe?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mkuchika, kama ifuatavyo:-

Katika maandalizi yetu ya kikao ambacho tunatarajia kukifanya mwezi wa Septemba tayari tumeshakaa na wadau kwa maana ya sekta zinazohusika na pia hata sekta ambazo ziko nje ya mfumo wa Serikali ili kubaini maeneo ya ushirikiano ambayo yataleta tija katika nchi zetu mbili.

Kwa hiyo, napenda kumhakikishia kwamba hilo tunalifanya na ndiyo utaratibu tulionao kwamba tunapoandaa mikutano yetu hii ya tume kuwa tunashirikisha Wizara zote, sekta zote na pia sekta binafsi ambayo inamchango mkubwa sana katika biashara.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kufidia muda tunaendelea kidogo kama dakika tatu hivi. Kwa hiyo, swali la nyongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. JENISTA MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika kipindi chote ambacho Tume hii imekuwepo na imekuwa ikifanya kazi wakati huo huo tumekuwa na Jumuiya ya Kirafiki kati ya Tanzania na Msumbiji kama inavyotambulika kwa jina la *Tanzania and Mozambique Friendship Association (TAMOFA)*, ambayo imekuwa ikifanya kazi nzuri sana ya kujenga mahusiano hayo ya kisiasa na kiuchumi na mifamo mizuri ipo katika Mkoa wa Mtwara na Mkoa wa Ruvuma hususani katika Wilaya ya Songea Vijijini, Jimbo la Peramiho mambo mengi sana yalifanyika na Jumuiya hiyo.

Je, Serikali sasa iko tayari wakati inapendelea na mipango ya tume kuimairisha tena Jumuiya hiyo ya kirafiki ili ziweze kushirikiana kwa pamoja kukuza mahusiano hayo ya kisiasa na kiuchumi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Ni kweli ipo ya Jumuiya hiyo ya kirafiki kati ya wananchi wa Tanzania na wa Msumbiji ijulikanayo kama *TAMOFA*. Jumuiya hii ni Jumuiya isiyo ya kiserikali, lakini ni Jumuiya mbayo inawajumuisha watu mbalimbali baadhi yao wakiwa ndani ya Serikali.

Sisi katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa tunaitambua Jumuiya hii tunaipongeza na tunatambua kazi nzuri anayofanya na katika maandalizi yetu ya kikao cha pamoja cha tume tutafanya jitihada pia ya kukaa na wenzetu walioko katika Jumuiya hii ili tuweze kubeba yale ambayo yatakuwa na manufaa katika nchi zetu mbili.

Lakini nichukue fursa hii kumpongeza kwanza Mheshimiwa George Mkuchika na Mheshimiwa Jenista Mhagama mwenyewe kwa kuweza kuwa mstari wa mbele katika kuimarisha shughuli za ushirika huu wa pamoja wa kirafiki kati ya Tanzania na Msumbiji yaani *TAMOFA*.(*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha, Katibu endelea na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2005 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2006/2007

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita mtoa hoja ninalo tangazo. Nimeanza kupata karatasi za maombi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uchumi. Lakini kwa utaratibu wetu ni kwamba hoja hii ikishatolewa leo kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ni utaratibu wetu kwamba hoja hii pamoja na ile itakayofuata saa kumi ya Mheshimiwa Waziri wa fedha zitaanza kujadiliwa kwa pamoja siku ya jumatatu. Kwa hiyo, sasa maombi yaje na yaendelee kuja lakini natoa taarifa kwamba baada ya mtoa hoja asubuhi hii nitasitisha shughuri za Bunge ili tusubiri hotuba ya saa kumi ya Waziri wa Fedha. Baada ya hapo nitaarisha Bunge hadi Jumatatu ili yote mawili Uchumi na Fedha yaweze kujadiliwa. Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili Taarifa ya hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2005 na mapendekezo ya mpango wa muda wa kati na mfumo wa matumizi ya Serikali kwa

kipindi cha mwaka 2006/2007 hadi 2008/2009. Pamoja na hotuba hii nimewasilisha leo asubuhi kupitia Naibu Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji kitabu cha hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2005 na kitabu cha mpango wa maendeleo kwa mwaka 2006/2007. Awali ya yote napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kiwete, pamoja na Makamu wake Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuchanguliwa kwao kwa ushindi mkubwa wa kishindo. Aidha napenda kumpongeza Mheshimiwa Aman Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kwake kwa kipindi cha pili kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu katika awamu ya nne. Aidha napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Samuel John Sitta, Mbunge wa Urambo Magharibi, Naibu Spika, Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini, kwa kuchaguliwa kwenu kuwa Wabunge na kushika nyadhifa hizo za juu katika Bunge letu la awamu ya nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia, Mawaziri wenzangu wote pamoja na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kwa kushika nyadhifa hizo. Mwisho napenda kuwapongeza Wabunge wote kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kwao kuingia katika Bunge hili Tukufu. Aidha nawashukuru kipekee wapiga kura wangu wa Jimbo la Ulanga Magharibi, kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kunichagua kwa mara ya tatu kuwa Mbunge wao. Nitaendelea kushirikiana wao kuliletea maendeleo Jimbo letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, ikiongozwa na Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kutupatia ushauri na maelekezo wakati wa kujadili muhtasari wa hotuba hii.

Aidha nawashukuru wale wote tulioshirikiana nao katika maandalizi ya taarifa hii na mpango ninaouwasilisha leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, timu yote ya wataalam wa Wizara na Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ikiongozwa na Katibu Mkuu. Dr. Enos Bukuku na Naibu wake Dr. Stagomena Tax Bamwenda, pamoja na wataalam wa Wizara na Taasisi mbalimbali kwa michango yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba nianze kutoa muhtasari wa mapitio ya hali ya uchumi na maendeleo ya mwaka 2005 ikiwa ni mapitio ya mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania. Maarufu kwa MKUKUTA wenye muelekeo na azma ya kutufikisha kwenye malengo ya jumla ya dira ya taifa ya maendeleo 2020.

Kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 Bajeti iliendelea kujikita zaidi katika kuendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii yaliyolenga katika kukuza na kutengemaza uchumi kwa kutekeleza sera, mipango, programu na mikakati mbalimbali ya kuharakisha

maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya taifa letu. Aidha ikumbukwe kwamba taarifa hii ni ya kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba, 2005 na sehemu chache zimegusia robo ya kwanza ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya hali ya uchumi kwa ujumla. Pato la Taifa, katika mwaka 2005, pato la taifa lilikuwa kwa asilimia 6.8, ikilinganishwa na lengo la ukuaji la asilimia 6.9 na ukuaji halisi wa asilimia 6.7 mwaka 2004. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na ukuajia wa sekta za uuzaji wa jumla, rejareja na mahoteli ikijumuisha watalii, bidhaa za viwandani, ujenzi, madini na uchimbaji mawe na mawasiliano na uchukuzi. Vilevile mchango mwingine ulitokana na ongezeko la viwango vya ukuaji wa sekta vya umeme na maji, huduma za kibiashara na fedha na uendeshaji wa Serikali na huduma nyingine. Pamoja na mambo mengine ukuaji huu haukufikia lengo kutokana na ukame uliotokea katika maeneo mengi nchini hasa katika kipindi cha robo ya nne ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, pato la wastani kwa kila mtu liliongezeka hadi shilingi 360,865 mwaka 2005 kutoka shilingi 319,754 mwaka 2004, kwa bei za miaka husika, sawa na ongezeko la asilimia 12.9. Aidha kwa bei za mwaka 1992, wastani ulikuwa ni shilingi 61,798 mwaka 2005 ikilinganishwa na shilingi 54,335 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 4.2.

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa uliendelea kupungua kidogo kidogo ambapo mchango wa sekta nyingine hasa bidha za viwandani, uuzaji wa jumla, rejareja na mahoteli ikijumuisha utalii, madini na ujenzi uliendelea kuongezeka. Hali hii inaonyesha kubadilika kwa muundo wa uchumi ambao sasa hautegemei kuchangiwa kwa kiasi kikubwa na kilimo pekee. Hata hivyo mchango wa sekta ya kilimo kwa pato la taifa uliendelea kuwa mkubwa ikilinganishwa na sekta nyingine. Katika mwaka 2005 sekta ya kilimo ilichangia asilimia 45.6 ya pato la taifa ikilinganishwa na asilimia 46.3 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005, sekta ya kilimo ilikuwa kwa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 8.8 mwaka 2004. Kupungua kwa ukuaji wa sekta hii kulitokana hasa na kushuka kwa uzalishaji katika sekta ndogo za mazao na mifugo. Ukuaji wa sekta hizi ndogo ulishuka kutoka asilimia 6.0 na 4.8 mwaka 2004 hadi asilimia 5.2 na 4.2 mwaka 2005 kwa mtiririko huo. Hata hivyo viwango vya ukuaji wa sekta ndogo za uvuvi na misitu na uwindaji viliongezeka kutoka asilimia 6.7 na 3.8 mwaka 2004 hadi asilimia 7.3 na 4.5 mwaka 2005 kwa mtiririko huo.

Mheshimiwa Spika, Sekta za bidhaa za viwandani ilikuwa kwa asilimia 9 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 8.6 mwaka 2004. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa katika baadhi ya viwanda hususani saruji, aluminiam na bati. Mchango wa sekta ya uzalishaji bidhaa viwandani uliongezeka hadi kufikia asilimia 9 mwaka 2005 kutoka asilimia 8.8 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mahoteli, uuzaji jumla na rejareja ikijumuisha utalii ilikuwa kwa asilimia 8.2 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 7.8 mwaka 2004.

Mchango wa sekta hii katika pato la taifa ulikuwa kwa asilimia 17.2 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 16.9 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, sekta ya madini na uchimbaji mawe ilikuwa kwa asilimia 15.7 mwaka 2005 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 15.4 mwaka 2004. Kuongezeka kwa ukuaji wa sekta hii kulitokana hasa na uwekezaji mpya katika machimbo ya dhahabu ya Tulawaka yaliyoko Wilaya ya Biharamulo Mkoa wa Kagera. Mchango wa sekta ya madini na uchimbaji mawe katika pato la taifa uliongezeka hadi asilimia 3.5 mwaka 2005 kutoka asilimia 3.2 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta ya ujenzi katika pato la taifa ulikuwa kwa asilimia 5.7 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2004. Sekta ilikuwa kwa aslimia 11.9 mwaka 2005 kutoka asilimia 10.8 mwaka 2004. Ukuaji huu ulitokana hasa na ujenzi wa majengo yasiyo ya kuishi na nyumba za kuishi, ujenzi wa barabara na madaraja, pamoja na uendelezaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mawasiliano na uchukuzi ilikuwa kwa asilimia 6.4 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 6 mwaka 2004. Ukuaji huu ulitokana na kuboreshwa kwa miundo mbinu ya usafirishaji na kuongezeka kwa huduma za mawasiliano hasa kwa njia za simu. Hata hivyo mchango wa sekta ya mawasiliano na uchukuzi katika pato la taifa ulibakia kuwa asilimia 5.4 mwaka 2005 kama ilivyokuwa mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, sekta ya umeme na maji ilikuwa kwa asilimia 5.1 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2004. Kuongezeka kwa ukuaji huu kulitokana na kukua kwa sekta ndogo za umeme na maji kutoka asilimia 4.7 na 2.8 mwaka 2004 hadi asilimia 5.3 na 3.4 mwaka 2005 kwa mtiririko huo. Mchango wa sekta ya umeme na maji katika pato la taifa ulibakia kuwa asilimia 1.6 kama ilivyokuwa mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, sekta ya huduma za fedha na kibiashara ilikuwa kwa asilimia 5.3 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2004. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka katika ukuajia wa sekta ndogo za fedha na bima, upangishaji majengo na huduma za kibiashara wa asilimia 5.7, 5.0 na 6.1 mwaka 2005 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.4, 4.3 na 5.5 mwaka 2004 kwa mtiririko huo. Sekta hii ilichangia asilimia 9.6 katika pato la taifa mwaka 2005 ikilinganishwa na asimilia 9.7 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya uendeshaji Serikali na huduma nyingine ilikua kwa asilimia 5.1 mwaka 2005, kutoka asilimia 4.3 mwaka 2004. Ukuaji huu ulichangiwa na sekta ndogo ya utawala kwa asilimia 4.7 mwaka 2005, kutoa asilimia 2.8 mwaka 2004. Sekta ndogo za elimu, afya na huduma nyinginezo zilikua kwa asilimia 6.3, 5.7 na 4.9, viwango ambavyo ni pungufu ya vile vilivyofikiwa katika mwaka 2004 vya asilimia 6.6, 6.0 na 5.8, kwa mtiririko huo. Mchango wa sekta ya uendeshaji Serikali na huduma nyingine katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.0 mwaka 2005, ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2004.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri samahani si jambo la kawaida, lakini ningekuomba uketi kwanza nitoe maelezo. Naona tuna tatizo kubwa la mwanga katika ukumbi huu. Kwanza ninazo karatasi zinazolalamika kwamba mwanga ni mkali. Tumepunguza sasa ninazo nyingi zaidi zinasema sasa ni giza, sasa nimemwagiza Katibu baadaye tutakapositisha shughuli za leo asubuhi na ile saa kumi akae na wataalamu waweze kuleta hali ambayo labda itakuwa katikati ya hapo. Kwa sasa hivi nitaomba kwa sababu sehemu ya *front bench* kabisa na Mawaziri ndio hawezi hata kusoma karatasi itabidi tuwashe taa ili waweze kuona. (*Makofi*)

Marekebisho mengine ya mwanga mkali yatafanyika baadaye, samahani sana Mheshimiwa Waziri, warekebishe hizo taa.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa nyingine.

Mheshimiwa Spika, Kasi ya Upandaji Bei, katika mwaka 2005, wastani wa kasi ya upandaji bei ulikuwa asilimia 4.3 ikilinganishwa na lengo la asilimia 4.0 na kasi halisi ya asilimia 4.2 mwaka 2004. Kuongezeka kwa kasi ya upandaji bei kulitokana na kupanda kwa bei ya bidhaa za chakula kutokana na hali ya ukame na kupanda kwa wastani wa bei za mafuta ya petroli zilizosabasiha kuongezeka kwa gharama za usafirishaji na umeme. Aidha kwa mwezi Machi 2006 kasi ya upandaji bei ilifikia asilimia 6.9 kupanda huku kulitokana na ukame uliopandisha bei ya vyakula na gharama za umeme.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali, Mapato, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2005/2006, mapato ya ndani yalifikia shilingi 1,013.8 bilioni, ikilinganishwa na shilingi 869.9 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2004/2005. Mapato hayo ni sawa na wastani wa shilingi 169 bilioni kwa mwezi ikilinganishwa na shilingi 145 bilioni kwa mwezi katika kipindi kama hicho mwaka 2004/2005 sawa na ongezeko la asilimia 16.6. Kuongezeka kwa mapato kulitokana hasa na kuendelea kuimarika kwa usimamizi wa ukusanyaji wa kodi, hususan kodi ya mapato na ya ongezeko la thamani kwa bidhaa za ndani na nje. Kufikia Machi, 2006 mapato ya ndani yalikuwa shilingi 1,544.4 bilioni, sawa na asilimia 100.5 ya lengo katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Matumizi, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2005/2006, matumizi yalifikia shilingi 2,122.9 bilioni, ilikilinganishwa na shilingi 1,641.3 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2004/2005. Hadi Machi 2006, matumizi yalifikia shilingi 3,180.5 bilioni ikilinganishwa na makisio ya shilingi 3,171.1 bilioni sawa na ziada ya asilimia 0.3. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,199.6 bilioni zilitumika kwa matumizi ya kawaida na shilingi 980.9 bilioni kwa miradi ya maendeleo. Ongezeko la matumizi lilitokana na kuongezeka kwa gharama za uchaguzi kufuatia kuahirishwa kwa Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba na kufanyika tarehe 15 Desemba, 2005; kutoa ruzuku kwa *TANESCO* kwa ajili ya kununua *"transformer"* ya kituo cha Ilala, Jijini Dar es Salaam baada ya iliyokuwepo kuungua; na gharama za kulikwamua Shirika la Ndege Tanzania. Aidha, mahitaji mengine yaliyochangia katika ongezeko la matumizi yalitokana na maamuzi ya Serikali yaliyofanywa baada ya Bajeti kupitishwa, kama vile marekebisho ya

viwango vya posho za askari *(ration allowances),* pamoja na marekebisho ya mishahara ya watumishi wa afya.

Mheshimiwa Spika, Ujazi wa Fedha na Karadha, katika mwaka 2005, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana ($M_2$) uliongezeka kwa asilimia 36.2, ikilinganishwa na asilimia 19.2 mwaka 2004, ambapo ujazo wa fedha na tafsiri pana zaidi $(M_3)^2$ uliongezeka kwa asilimia 38.2 mwaka ulioishia Desemba 2005, kutoka asilimia 19.3 Desemba 2004. Ongezeko hilo lilikuwa zaidi ya lengo la asilimia 24 kwa $M_2$ na lengo la wigo wa asilimia 23-24 kwa $M_3$ katika mwaka 2005/2006. Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na ongezeko la amana za hundi, amana za akiba katika benki na kuongezeka kwa mikopo iliyotolewa na benki kwa sekta binafsi. Aidha, wastani wa viwango vya riba uliongezeka kidogo kutoka asilimia 14.8 mwaka 2004 hadi asilimia 15.0 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Ukuzaji Rasilimali, ukuzaji rasilimali uliongezeka kufikia shilingi 735,180 milioni mwaka 2005 kutoka shilingi 624,371 milioni mwaka 2004 kwa bei za mwaka 1992, sawa na ongezeko la asilimia 17.7.

Ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika uliongezeka kutoka shilingi 2,598,974 milioni mwaka 2004 hadi shilingi 3,149,402 milioni mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 21.2. Kuongezeka kwa ukuzaji rasimali kulitokana hasa na ujenzi wa majengo; uagizaji wa vifaa; na kuongezeka kwa shughuli nyinginezo za ukuzaji rasilimali zikiwemo uendelezaji ardhi, barabara na madaraja, pamoja na maji. Aidha, uwiano wa ukuzaji rasilimali na Pato la Taifa ulikuwa asilimia 32.9 ikilinganishwa na asilimia 29.8 mwaka 2004, kwa bei za mwaka 1992.

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta binafsi katika ukuzaji rasilimali ulikuwa asilimia 65.1 mwaka 2005, ikilinganishwa na asilimia 62.4 mwaka 2004. Kwa upande wa sekta ya umma, ukuzaji rasilimali uliongezeka hadi shilingi 1,068,171 milioni kutoka shilingi 950,077 milioni mwaka 2004 kwa bei za miaka husika, sawa na ongezeko la asilimia 12.4. Mchango wa sekta ya umma katika ukuzaji rasilimali kwa jumla ulikuwa asilimia 33.9 mwaka 2005, ikilinganishwa na asilimia 36.6 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Mikopo Kutoka Benki za Biashara kwa Sekta Mbalimbali, Mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa sekta mbalimbali iliongezeka kutoka shilingi 965,985.9 milioni mwaka 2003/2004 hadi shilingi 1,219,305.6 milioni mwaka 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 26.2. Kufikia mwishoni mwa Desemba 2005, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka hadi shilingi 1,425,062.3 milioni, ikilinganishwa na shilingi 1,060,077.3 milioni mwishoni mwa Desemba 2004. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 34.4 ikilinganishwa na asilimia 30.0 mwishoni mwa Desemba 2004.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka kufikia Dola za Kimarekeni milioni 1,676.3 mwaka 2005 kutoka Dola za Kimarekani milioni 1,473.1 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 13.8. Thamani ya mauzo ya bidhaa asilia iliongezeka na kufikia Dola za Kimarekani milioni 354.4 mwaka 2005 kutoka Dola za Kimarekani milioni 297.8 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 19.

Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya mazao ya Kahawa, Tumbaku na Pamba. Thamani ya mauzo ya bidhaa zisizo asilia iliongezeka na kufikia Dola za Marekani milioni 1321.8 mwaka 2005 kutoka Dola za Kimarekani milioni 1,175.3 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 12.5

Mheshimiwa Spika, bidhaa zisizo asilia zilichangia asilimia 78.8 ya mauzo yote wakati bidhaa asilia zilichangia asilimia 21.2. Pamoja na mafanikio hayo, mapato yatokanayo na mauzo nje yamekuwa na uwezo wa kugharimia asilimia 63.0 tu ya uagizaji nje. Changamoto iliyopo ni kuongeza mauzo nje na kuhamasisha uzakilishaji na uuzaji wa bidhaa zenye viwango vya kuweza kuhimili ushindani kama kahawa ya Kilicafe ya Kilimanjaro na Mbogamboga za *Gomba Estate* ya Arusha zinazouzwa katika Masoko yenye bei nzuri nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 2339.7 mwaka 2004 hadi Dola za Kimarekani milioni 2661.8 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 13.8. Thamini ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ilikuwa kubwa kuliko thamani ya bidhaa zilizouzwa nje na hivyo kuleta nakisi kubwa katika urari wa biashara na bidhaa.

Mheshimiwa Spika, thamani ya bidhaa za matumizi ya kawaida ilipungua kwa asilimia 1.8 kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula hususan mahindi. Uagizaji wa bidhaa nyingine za matumizi ya kawaida uliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 515.9 mwaka 2004 hadi Dola za Kimarekani milioni 583 mwaka 2005 sawa na ongezeko la asilimia 13.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005 urari wa malipo yote ulikuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani milioni 437.5 ikilinganishwa na ziada ya Dola za Kimarekani milioni 43.4 katika mwaka 2004. Nakisi hii ilitokana na kuongezeka kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa ambapo mwaka 2005 urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya Dola za Kimarekani 985.5 sawa na asilimia 13.7, ikilinganishwa na nakisi ya Dola za Kimarekani 866.6 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni ilipungua hadi Dola za Kimarekani milioni 2,048.4 mwaka 2005 kutoka Dola za Kimarekani milioni 2296.1 mwaka 2004 sawa na upungufu wa asilimia 10.8. Kiasi cha akiba ya fedha za kigeni mwaka 2005 kilikuwa na uwezo wa kuagiza bidhaa na kulipia huduma miezi 6.4 ikilinganishwa na kiasi cha mwaka 2004 kilichokuwa na uwezo wa miezi 8.2. Kiasi hiki ni chini ya lengo lililokusudiwa la uwezo wa kuagiza bidhaa na kulipia gharama kwa zaidi ya miezi saba.

Mheshimiwa Spika, thamani ya Shilingi imeendelea kufuata mabadiliko ya hali ya soko. Mwaka 2005 thamani ya Shilingi ya Tanzania ilikuwa na wastani wa Shilingi 1,128.8 kwa Dola moja ya Kimarekani, ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 1,089.3 kwa Dola moja ya Kimarekani mwaka 2004. Hali hii inaonyesha kushuka kwa thamani ya Shilingi kwa aslimia 3.6 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2004. Aidha, hadi

mwisho mwa Desemba, 2005, thamani ya Shilingi kwa Dola moja ya Kimarekani ilikuwa Shilingi 1,165.5 ikilinganishwa na Shilingi 1,043.0 mwishoni mwa Desemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, misaada na Mikopo imeendelea kupatikana kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na kwamba Wahisani wengi wameonyesha kuitikia mwito wa kuisaidia nchi yetu katika kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Misaada na mikopo ya Bajeti ya kawaida ilifikia Shilingi milioni 576,956 mwezi Machi, 2006 ikilinganishwa na makadirio ya Shilingi milioni 589,913 sawa na asilimia 97.8.

Upungufu huu ulitokana na baadhi ya nchi Wahisani pamoja na Benki ya Dunia kupunguza misaada na mikopo pamoja na wengine kuchelesha utoaji wa misaada na mikopo yao hasa ile ya *Basket Funding*. Hata hivyo, idadi kubwa ya Wahisani walitoa misaada waliyoahidi. Kwa upande wa misaada na mikopo kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo Shilingi milioni 731,711 zilipatikana ikilinganishwa na Shilingi milioni 783,467 zilizoahidiwa , sawa na asilimia 80.7.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2005 Deni la Taifa lilifikia Dola za Kimarekani milioni 9,961.3 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 9,726.9 ilipofika Desemba, 2004, sawa na ongezeko la asilimia 2.5. Kati ya deni hilo, Dola za Kimarekani milioni 7,934.4 ni deni la nje sawa na asilimia 79.6 ya deni lote. Dola za Kimarekani milioni 226.9 ni deni la ndani. Deni la nje lilipungua kwa asilimia 1.1, ikilinganishwa na mwaka 2004 ambapo lilikuwa Dola za Kimarekani milioni 8,022.9. Kiasi hicho cha deni la nje kinahimilika, licha ya kuwa kikubwa kutokana na malimbikizo ya riba kwa madeni ambayo hayajasamehewa na nchi zisizo wanachama wa *Paris Club*.

Pamoja na kuzingatia tahadhari ya mzigo wa madeni, hatuwezi kusita kukopa mikopo nafuu na stahimilivu, ambayo itaelekezwa katika kuchangia kujenga uwezo wa uchumi na kuongeza uwekezaji, hatimaye kuibua ongezeko la ajira, mauzo nje, mapato ya Serikali, kuboresha miundombinu na maendeleo ya rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, Ulipaji wa deni la nje uliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 77.8 mwaka 2004, hadi Dola za Kimarekani milioni 91.1 mwaka 2005. Deni hilo lilijumuisha mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 53.4 na riba ya Dola za Kimarekani milioni 37.7. Kuongezeka huko kulitokana na ulipaji wa madeni ambayo hayajasamehewa na nchi sisizo wanachama wa *Paris Club*.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2005, deni la ndani lilifikia Shilingi bilioni 2,362.5, ikilinganishwa na deni la Shilingi bilioni 1,813.1, katika kipindi kama hicho mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 30.3. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali. Kiasi cha Shilingi bilioni 716.8 za deni la ndani zililipwa katika mwaka 2005. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 616.4 zilikuwa ni mkopo na Shilingi bilioni 100.4 ilikuwa ni riba.

Mheshimiwa Spika, pato la dunia lilikua kwa asilimia 4.8 mwaka 2005, ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2004. Kushuka kwa ukuaji wa pato la dunia kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuyumba kwa uchumi wa nchi zilizoendelea hasa katika Bara la Ulaya hususan Ufaransa, Ujerumani, Italia na Uingereza; pamoja na ongezeko kubwa la bei ya mafuta na majanga mbalimbali yaliyoikumba dunia. Pamoja na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia, baadhi ya nchi za Asia zinazochipukia kiviwanda zilikuwa na ukuaji wa haraka wa uchumi, kwa mfano ukuaji wa uchumi wa China ulifikia asilimia 9.9 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, pato la nchi zilizoendelea lilikua kwa asilimia 2.7 mwaka 2005, ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2004. Kushuka kwa ukuaji wa pato la nchi zilizoendelea kulichangiwa hasa na kupanda kwa bei za mafuta na kupungua kwa mauzo nje.

Kwa upande wa nchi zinazoendelea na nchi za Asia zinazoinukia kiviwanda, wastani wa pato lilipungua hadi asilimia 7.2 na 8.6 kwa mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 7.6 na 8.8 mwaka 2004, kwa mtiririko huo. Ukuaji wa pato la nchi zinazoendelea, ikilinganishwa na ukuaji wa pato la dunia, umeendelea kuimarika kutokana na kukua kwa biashara na shughuli za uzalishaji viwandani na utekelezaji mzuri wa sera za kurekebisha uchumi.

Mheshimiwa Spika, pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara lilikua kwa wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2005, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2004. Mwaka 2005, ukuaji wa pato la Bara la Afrika ulishuka hadi wastani wa asilimia 5.2 kutoka wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2004.

Ukuaji wa pato la Bara la Afrika ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya mafuta, madini na ongezeko la bei kwa baadhi ya bidhaa za kilimo. Aidha, utekelezaji wa sera na mageuzi ya kiuchumi kwa baadhi ya nchi barani Afrika kulichangia katika ukuaji huo. Hata hivyo, ukuaji ulipungua kutokana na matatizo ya ukame na migogoro ya kisiasa iliyozikumba baadhi ya nchi za Kiafrika.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi za Maziwa Makuu ikiwemo Tanzania, pato lilikua kwa wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2005, sawa na kiwango cha mwaka 2004. Kwa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki pato lilikua kwa wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2005, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2004. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya madini na ongezeko la bei kwa baadhi ya bidhaa za kilimo. Kwa upande wa nchi za Afrika ya Kati na Magharibi, pato lilikua kwa wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2005, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.6 mwaka 2004.

Hivyo, ukuaji wa asilimia 6.8 wa pato la Taifa letu kwa mwaka 2005 ni hatua nzuri zaidi siyo tu katika kanda hii ya Afrika Mashariki na kati, bali pia katika Kanda yote ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hii siyo kujipigia debe ingawa hili siyo baya; ni suala la kuwa na mikakati mizuri ya kukuza uchumi na maendeleo ya jamii ikijumuisha juhudi kubwa za kuvutia wawekezaji kwa kujenga na kuboresha kuboresha

mazingira ya biashara nchini. Juhudi zitaendelezwa kwa kasi na nguvu zaidi katika miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, uhusiano wa nchi yetu na mataifa mengine duniani pamoja na mashirika ya kimataifa na ushirikiano wa kikanda umeendelea kuimarika kwa kiwango kikubwa na hivyo kuendelea kulijengea Taifa letu mazingira mazuri ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya Ushuru wa Pamoja wa Forodha kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ilianza kutumika tarehe 01 Januari, 2005 baada ya kusainiwa na Marais wa nchi wanachama wa Jumuiya na kuridhiwa na Mabunge ya nchi hizo.

Aidha, Jumuiya iliendelea kuandaa Mkakati wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Mkakati huo unafuatia kukamilika kwa kipindi cha mkakati wa awali wa mwaka 2001 - 2005 ambao kwa kiasi kikubwa ulifanikisha kuanzishwa kwa Ushirikiano wa Ushuru wa Pamoja wa Forodha, pamoja na kuweka misingi ya kuanzishwa kwa Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo, Jumuiya iliendelea kutekeleza shughuli za Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Ziwa *Victoria* kama ifuatavyo:-

Mradi wa Ushirikiano wa Uvuvi katika Ziwa *Victoria*, Matayarisho ya miradi ya miundombinu ikijumuisha barabara, reli, usafiri wa majini, uzalishaji na usambazaji wa nishati na miradi ya kilimo. Aidha, katika kutimiza azma ya kuwa na majengo ya kudumu, maandalizi ya ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya yalifikia hatua nzuri baada ya Tanzania kutoa eneo, pamoja na Mshauri Mwelekezi wa ujenzi kupatikana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005, Mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa Mkutano wa Kimataifa kuhusu Eneo la Maziwa Makuu ulifanyika Lusaka Zambia chini ya Uenyekiti wa Tanzania. Mkutano huo ulijadili Itifaki ya mpango na programu za muda mfupi, kati na mrefu na kupitisha miradi inayokusudiwa kutekelezwa kwenye maeneo makubwa manne yafuatayo nayo ni Amani na Usalama, Demokrasia na Utawala Bora, Maendeleo ya kiuchumi na ushirikiano kikanda, Haki za Binadamu na Masuala ya Kijamii. Aidha, katika mkutano huo nchi ya Misri ilikubaliwa kuwa mwanachama wa nchi za eneo la Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*); Katika mwaka 2005, *SADC* ilifikisha miaka 25 tangu kuanzishwa kwake. Mambo yaliyofanyika katika kipindi cha 2005/06 ni pamoja na kupitisha Azimio la kuongeza lengo la chini la ushiriki wa wanawake katika maamuzi ya kisiasa na uongozi wa ngazi za juu kutoka asilimia 30 hadi asilimia 50 ifikapo mwaka 2010 ikiwa ni sambamba na malengo ya Jumuiya ya Afrika, kupitisha uamuzi wa kujenga Makao Makuu ya *SADC* Gaborone, Botswana katika kipindi cha miaka kumi na mitano na kukubaliana juu ya taratibu zinazohusu utatuzi wa migogoro ya kibiashara kwa lengo la kurekebisha na kuboresha Itifaki ya biashara ya *SADC*.

Aidha, taratibu za kuunganisha njia za umeme kati ya Tanzania na Zambia *(Zambia–Tanzania Inter-connector)* ziliendelea kukamilishwa na Sekretariati ya *SADC* baada ya fedha za kutekeleza mradi kupatikana ili Tanzania iweze kuunganishwa rasmi kwenye mradi wa *Southern African Power Pool* (*SAPP)* kama nchi nyingine za *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango Mpya wa Ushirikiano Ili Kuleta Maendeleo Afrika *(NEPAD)*, Serikali ilitoa mwaliko kwa Sekretariati ya *African Peer Review Mechanism* kuja nchini kuhakiki ni kwa jinsi gani Tanzania inatekeleza makubaliano yaliyofikiwa chini ya *NEPAD* ambayo yanajumuisha utawala wa sheria, haki za binadamu, uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa Vyama vya Siasa, mageuzi katika uchumi yenye kulenga katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini na kuendeleza ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi. Haya ni matokeo ya mkataba wa kujiunga na utaratibu unaotoa fursa kwa nchi kujitathmini na kujipima zenyewe kuhusiana na utekelezaji wa vigezo muhimu vya *NEPAD*, ulioridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Februari, 2005.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mageuzi ya kiuchumi yanayoendelea hapa nchini kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Serikali iliwasilisha miradi ifuatayo kwa Sekretariati ya *NEPAD*:- Ujenzi wa daraja la Umoja linalounganisha nchi za Tanzania na Msumbiji, upanuzi wa Bandari ya Dar es salaam, uunganishaji wa umeme kutoka Zambia hadi Kenya, maendeleo ya ukanda wa Mtwara na uboreshaji wa barabara za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikiano wa Kiufundi Baina ya Nchi Zinazoendelea; Katika mwaka 2005 Tanzania iliendelea kutumia fursa mbali mbali zilizotolewa na Serikali ya China chini ya mpango wa ushirikiano kwa nchi zinazoendelea zinazosaidiwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa. Wataalam wa Kitanzania kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali walihudhuria mafunzo ya Uvunaji wa Maji ya Mvua, Nishati Mbadala na Televisheni nchini China.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maendeleo ya Sekta, Kilimo; Mwaka 2005/2006, uzalishaji wa mazao ya chakula ulipungua kwa baadhi ya mazao yakiwemo Ngano, Mahindi, Mtama na Ndizi. Uzalishaji uliongezeka kwa mazao mengine kama Muhogo, Kunde na Mpunga. Kwa upande wa mazao ya biashara uzalishaji uliongezeka kwa mazao ya Pareto, Tumbaku na Pamba, wakati ambapo uzalishaji wa kahawa na korosho ulipungua. Aidha, eneo lililo chini ya kilimo cha umwagiliaji lilipungua kutoka hekta 23,970 mwaka 2004, hadi hekta 22,506, mwaka 2005.

Kupungua kwa uzalishaji kwa baadhi ya mazao kulitokana na ukame, huduma duni za ughani na hali ya bei za mazao kwa wakulima ambazo hazitabiriki. Hivyo kuanzia sasa suala la kilimo cha umwagiliaji kama sehemu ya Mkakati wa Mapinduzi ya kilimo nchini kitapewa msukumo zaidi.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2006/2007, mkazo katika Sekta ya Kilimo utakuwa ni pamoja na kuendelea kuboresha upatikanaji wa chakula cha kutosha, kupanua kilimo cha umwagiliaji na kuongeza Hifadhi ya Taifa ya Chakula.

Mheshimiwa Spika, Viwanda: Mwaka 2005/2006, mafanikio ya kuridhisha yalipatikana katika Sekta ya Viwanda yakiwemo kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa kulingana na mahitaji ya soko la ndani na nje. Viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo cha chakula vilihamasika na kuanza kutumia teknolojia sahihi za uzalishaji na usindikaji wa bidhaa mbalimbali kama matumizi ya teknolojia ya *biogas*, teknolojia ya kukausha tumbaku kwa usalama zaidi, usindikaji wa mafuta ya kupikia na teknolojia ya kusafisha chumvi katika kiwango cha mataifa na kuimarishwa kwa Maabara ya upimaji ubora wa vyakula za Shirika la Viwango Tanzania *(TBS).*

Aidha, katika kuhamasisha uwekezaji katika ujenzi wa maeneo mapya ya kuzalisha bidhaa kwa ajili ya mauzo nje *(EPZ),* viwanda viwili vilianzishwa na kuanza uzalishaji. Viwanda hivyo ni *A-Z* kilichopo Kisongo-Arusha, kinachozalisha vyandarua vyenye dawa na Kiwanda cha *African Packaging System* kilichopo *Millenium Business Park* Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa mwaka 2006/2007, unalenga katika yafuatayo:-

Kwanza, kujenga uwezo wa sekta binafsi wa kuongeza thamani na ubora wa bidhaa kwa kuzingatia matakwa ya soko la kimataifa, kuongeza juhudi zaidi za kuhamasisha uanzishaji wa maeneo maalum ya uwekezaji na uzalishaji kwa ajili ya uuzaji nje (*EPZ*), kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Viwanda vya Nguo, Ngozi na Usindikaji Mazao ya Kilimo na Mifugo, kuboresha mazingira ya uzalishaji viwandani na kuimarisha mahusiano ya kiuchumi kati ya nchi yetu na jumuia za kikanda na kimataifa. Juhudi zitaongezwa katika mwaka 2006/07 kutumia fursa za masoko nafuu ya *AGOA, EBA, Canadian PACT* pamoja na yale ya Japan, Korea ya Kusini na China.

Mheshimiwa Spika, Madini: Katika mwaka 2005/2006, Sekta ya Madini imepata mafanikio ya kuridhisha yakiwemo kuanza kwa utekelezaji wa mfumo maalum unaolenga kuimarisha utoaji wa leseni za madini na kuongeza maduhuli ya Serikali, kukamilika kwa upimaji wa viwanja vidogo vya madini Mkoani Morogoro, kukamilika kwa ufungaji na kuanza kutumika mashine za kuchonga na kusanifu madini kwenye Kituo cha Uchongaji na Usafishaji Vito Arusha na kutoa elimu na mafunzo mbalimbali kwa wachimbaji wadogo. Mapato yatokanayo na madini hayaridhishi, hivyo Serikali imeunda kamati maalum ya kutathmini suala hili kwa kina.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2006/2007, Sekta ya Madini inalenga kuboresha mahusiano kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa, kuongeza nafasi za ajira, kuhakikisha uchimbaji salama na unaozingatia utunzaji mazingira, kuunda kitengo cha kuratibu maendeleo ya wachimbaji wadogo, kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza zaidi na kuhakikisha kwamba madini yanayozalishwa yanaongezewa thamani kabla ya kuzwa nje.

Mheshimiwa Spika, Nishati; Mafanikio yaliyopatikana mwaka 2005/06, katika sekta ya nishati ni pamoja na kuanza kwa uzalishaji umeme kwa kutumia gesi ya Songosongo, kusainiwa kwa makubaliano ya makusudio *(Agreement of Intent)* kati ya Serikali na mwekezaji wa mradi wa gesi ya *Mnazi Bay* utakaozalisha umeme wa *MW 14* kwa Mkoa wa Lindi na Mtwara na kukamilika kwa ufafiti uliofanyika mkoani Mwanza wa kubaini vikwazo katika kutumia umeme utokanao na jua kama nishati mbadala. Vilevile, *TANESCO* iliingia mkataba na kampuni ya *Wartisila* ili kurekebisha mtambo wa *IPTL* utumie gesi kuzalisha umeme badala ya mafuta ya petroli.

Mafanikio mengine ni pamoja na kukamilika kwa mradi wa umeme wa *Lower Kihansi*, kukamilika kwa miradi ya kupeleka umeme Wilaya za Serengeti na Ukerewe na kuendelea na mradi wa Umeme wa Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, sekta ya nishati inalenga kuendeleza miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya Songosongo. Kiasi cha umeme kinachotegemewa kuzalishwa ni *MW 45 (IPTL-Tegeta), MW 200 (Kinyerezi), MW 60* (Ubungo-Awamu ya Kwanza) na *MW 40* (Ubungo-Awamu ya Pili) na *MW 100* umeme wa kukodisha (*leasing*).

Aidha, malengo mengine ni pamoja na kununua umeme kutoka Zambia, kuandaa mkakati wa kuboresha uzalishaji na usambazaji umeme Mijini na Vijijini, kuongeza upatikanaji wa nishati mbadala Vijijini ili kupunguza uharibifu wa mazingira, kuendeleza jitihada za utafutaji mafuta ya petroli na kuongeza matumizi ya nishati itokanayo na mionzi ya jua. Mradi wa makaa ya mawe ya Kiwira utapanuliwa na Mwekezaji Binafsi kwa lengo la kuzalisha *MW 200* za umeme. Juhudi za kuongeza vyanzo vingine vya kuzalisha umeme badala ya kutegemea maji, zitapewa msukumo zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, kulikuwa na mafanikio yafuatayo katika Sekta ya Barabara. Barabara zenye urefu wa kilometa 10,062 za Mikoa na kilometa 5,968 za barabara kuu zilifanyiwa matengenezo na kuwa na hali nzuri, madaraja 699 yalifanyiwa matengenezo na 17 mapya yalijengwa na jumla ya makandarasi 315 walipatiwa mafunzo muhimu kwa lengo la kujengewa uwezo zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2006/2007 Serikali inalenga kutekeleza yafuatayo:-

Kukarabati jumla ya kilomita 15,000 za barabara za Mikoa na Wilaya, kuendeleza utekelezaji wa maalum wa kuboresha miundombinu katika Mikoa sita ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Kigoma, Rukwa na Tabora, kuendelea kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo na wadau wengine na kuzifanyia mapitio sera mbalimbali za sekta hii kwa lengo la kuziboresha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006 katika Sekta ya uchukuzi na mawasiliano, Serikali ilitekeleza yafuatayo:-

Kuendelea na ujenzi wa uwanja mpya wa ndege wa Songwe na kufikia asilimia 40, kukamilisha ukarabati wa njia za kuruka na kutua ndege katika viwanja vya Mwanza, Arusha na Kigoma, kuendelea na matengenezo ya miundombinu katika uwanja wa ndege wa Singida na kuendelea kukarabati magati katika bandari za Maziwa Makuu. Vile vile, kazi mbalimbali za ukarabati katika reli ya kati kwa lengo ya kuboresha huduma zimeendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Serikali inalenga kutekeleza yafuatayo:-

Kuanza kutekeleza mpango wa kubadilisha mfumo wa reli ya kati ikiwa ni pamoja na kubadilisha na kuweka mataruma ya uzito wa ratili 80, kuendeleza ujenzi wa na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege, bandari, magati, reli na mtandao wa mawasiliano, kuendeleza mpango wa kuoanisha viwango vya usafirishaji na mawasiliano vya ndani na vya kimataifa, kuboresha huduma za mamlaka ya hali na kuratibu vyombo vya usafiri wa abiria ili kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, teknolojia ya habari na mawasiliano. (TEKNOHAMA). Serikali katika mwaka 2005/2006 iliendelea kutoa kipaumbelea katika masuala ya TEKNOHAMA kwa kutekeleza yafuatayo:-

Kufanya tathimini kuhusu uendelezaji wa mkonga wa Taifa wa mawasiliano, kuunda timu ya waratibu wa TEKNOHAMA, kuanzisha Vituo vya Mawasiliano katika Miji ya Singida, Morogoro, Mtwara na Mpwapwa, Rungwe na Pemba na kuendelea kutekeleza mradi wa kujumuisha masomo ya TEKNOHAMA kwenye mitaala nchini *(e-schools, e-ducation, e-learning).*

Mheshimiwa Spika, malengo ya Serikali kwa kipindi cha 2006/2007 ni kama ifuatavyo:-

Kuendeleza teknolojia ya TEKNOHAMA, kuratibu utekelezaji wa shughuli za TEKNOHAMA na kuendeleza ushirikiano wa kikanda na mataifa katika nyanja za TEKNOHAMA.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 katika sekta ya maliasili Serikali, ilitekeleza yafuatayo:-

Jumla ya miche 66,182,502 ilioteshwa ikilinganishwa na miche 65,558,138 ya mwaka 2004. Ongezeko hilo sawa na asilimia 0.95 kukamilisha upimaji wa misitu ya hifadhi katika maeneo ya Kapingo, Engoma, Mikikagi na Itira katika Kisiwa cha Ukerewe na kukamilisha kazi za kuhesabu rasilimali za misitu katika Wilaya za Morogoro, Mvomero, Kilombero, Ulanga, Handeni, Kilindi, Kilwa, Nachingwea, Liwale, Tunduru, Mpanda na Rufiji.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Serikali katika mwaka 2006/2007 ni kuweka misingi madhubuti ya usimamizi wa rasilimali za maliasili ili kuongeza mchango wake

katika pato la Taifa, kuendeleza uhifadhi na uvunaji endelevu wa maliasili kwa kuboresha usimamizi na utendaji kazi unaofuata kanuni na sheria, kujenga mfumo madhubuti wa kiutawala ili kuboresha utoaji wa huduma na kupanua uwigo wa ushiriki wa sekta binafsi, mashirika yasiyo ya Kiserikali na wadau mbalimbali katika mipango inayohusu kulinda, kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa masuala mtambuka, katika mwaka 2005 Serikali iliendelea kutekeleza maamuzi mbalimbali ya kisera yanayozingatia masuala mtambuka. Nitaelezea kwa kifupi kuhusu utekelezaji wa masuala hayo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utawala Bora, Serikali iliendelea kutathimini hali ya rushwa hali ya rushwa kwa kutumia viashiria vilivyowekwa. Aidha, Serikali iliunda Kamati za maadili makazini pamoja na kuendelea kutayarisha mkakati wa pili wa kupambana na rushwa mahali pa kazi katika Ofisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 mambo yatakayosisitizwa ni kuendelea kuboresha usimamizi wa fedha za umma na uwabikaji, kushirikisha wadau mbalimbali katika mchakato wa maandalizi, ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera, mipango na mikakati ya maendeleo, kuendelea kutekeleza mpango wa maboresho ya Serikali za Mitaa, kuimarisha kampeni ya kupambana na rushwa, kupambana na wahalifu, kuendelea kurekebisha kanuni na sheria ikiwa ni pamoja na mfumo wa uendeshaji na kuimarisha upatikanaji wa taarifa zitakazosaidia kufanya maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vita dhidi ya Ukimwi, katika mwaka 2005, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo uhuishwaji wa shughuli za kudhibiti UKIMWI katika Wizara, Taasisi za Serikali na sekta binafsi na uandaaji wa mikakati ya kudhibiti UKIMWI kwa lengo la kuainisha shughuli zitakazofanyika katika kupambana na UKIMWI. Taarifa ya utafiti ya kila mwaka kuhusu UKIMWI na magonjwa ya zinaa (Oktoba 2005) inaonyesha kuwa maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI yameongezeka kutoka watu 188,140 mwaka 2004, hadi watu 188,400 mwaka 2005. Kati ya hao wanawake ni 97,130 sawa na asilimia 51.6

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005, mafunzo yaliendelea kutolewa katika ngazi mbalimbali. Mwongozo wa kudhibiti UKIMWI katika Sekta ya Umma uliandaliwa ambao uliweka bayana taratibu za kuzingatia wakati wa kutoa matunzo na msaada kwa watu waishio na virusi vya UKIMWI. Aidha, hadi Desemba 2005, vituo 96 vilikuwa vinatoa dawa za kurefusha maisha kwa watu waishio na virusi vya UKIMWI na watu 25,840 waishio na virusi vya UKIMWI walisajiliwa katika mpango wa matibabu na matunzo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2006/2007 Serikali itaendelea kuongeza idadi ya vituo vya kutolea dawa za kurefusha maisha kwa watu waishio na virusi vya UKIMWI na kuendelea kusajili watu waishio na virusi vya UKIMWI katika mpango wa matatibu na matunzo pamoja na kuendelea na juhudi za kutoa elimu katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya jinsia, katika mwaka 2005 Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kutekeleza sera, mipango na mikakati inayolenga katika kuboresha masuala ya jinsia, kuitunza, kujenga na kuendeleza malambo, visima na mabwawa katika maeneo ya wafugaji na wakulima, kuendeleza matumizi ya teknolojia sahihi za kuvuna, kuvuna, kuhifadhi na kusambaza maji ya mvua na ya ardhini kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji, kuhamasisha taasisi, wakulima wa tumbuku na watumiaji wengine wakubwa wa miti, kuni na mkaa, kwa mfano taasisi za elimu, majeshi na viwanda kuwa na mashamba yao ya miti, kuendelea kudhibiti uchomaji wa misitu na ukataji miti holela, kudhibiti shughuli za umwagiliaji na kupanda miti ifaayo kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Mipango maalum ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, katika muda wa kati, Serikali imeandaa kuendelea kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali inayojumuisha MKUKUTA, Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Mpango wa kurasimisha rasimamali na biashara Tanzania (MKURABITA) *Tanzania Mini-tiger Plan* 2020. *(TMTP 2020)* Mpango wa kuboresha Mazingira ya biashara Tanzania (MKUBITA) Mkakati wa madeni wa Taifa na Mkakati wa pamoja wa kusimamia misaada Tanzania. Aidha, Serikali imetayarisha mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUKUTA utakaotumika kufanya tathmini ya matokeo ya utekelezaji katika kipindi chote cha miaka mitano. Mfumo huu pia utabainisha mafanikio na mapungufu yatakayoweza kujitokeza ili kutoa maamuzi ya jinsi ya kuboresha uchumi na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 Serikali iliendelea kutekeleza mipango na mikakati hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA ulianza kutekelezwa mwaka 2005/2006 ambapo sekta zote na taasisi mbalimbali zilizoko za Serikali na zisizo za Serikali zinahusika katika utekelezaji wa maeneo makuu matatu ya MKUKUTA ambayo ni:-

(i) Ukuaji wa uchumi na upunguzaji wa umaskini wa kipato;

(ii) Uboreshaji wa maisha na ustawi wa jamii; na

(iii) Utawala bora na uwajibikaji. Baadhi ya mambo ya jumla ambayo yametekelezwa hadi sasa ni pamoja na kuoanisha MKUKUTA na mipango mikakati pamoja na bajeti ya Serikali, kukamilisha mwongozo wa jinsi ya kuoanisha mipango ya sekta na MKUKUTA na kukamilisha utayarishaji wa Mfumo wa ufuatiliaji wa hali ya umaskini kitaifa na kuelimisha Mikoa na Halmashauri za Serikali za Mitaa kuhusu mwongozo wa uoanishaji wa mipango ya sekta na MKUKUTA.

Aidha, zoezi la kuainisha gharama za utekelezaji wa malengo ya MKUKUTA lilianzishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2006/2007, Serikali itaendelea na zoezi la kuainisha gharama za utekelezaji wa malengo ya maeneo yote ya MKUKUTA na kuendelea na utekelezaji wa mipango, programu na mikakati mbalimbali ya kufanikisha malengo ya jumla ya MKUKUTA. Vile vile, zoezi la kuainisha gharama za utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 litaanzishwa rasmi katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza MKUBITA kwa lengo la kupunguza gharama za uanzishwaji na uendeshaji wa biashara kwa kuondoa vikwazo vikiwemo vya kisera, kisheria, kanuni, kiutaratibu na kitaasisi ambavyo vinakwamisha ukuaji wa sekta binafsi. Katika mwaka 2005/2006 MKUBITA uliendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini. Hii ilikuwa ni pamoja na kukamilisha mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali kwa lengo la kuimarisha mazingira ya biashara nchini. Aidha, uwakilishi wa wanawake umeendelea kuongezeko kutokana na marekebisho yalifanywa katika Katibu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kuendelea kurekebisha sheria za uchaguzi ili kuwa na uwakilishi wa Wabunge wanawake unaofika asilimia 30.

Aidha napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwateua wanawake wengi katika nyadhifa nyeti za kufanya maamuzi makubwa Serikalini. Kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge, wanawake wamefikia asilimia 30.41 ikiwa ni zaidi ya lengo la kiwango cha chini kilichowekwa kwenye Katiba ya nchi yetu na makubaliano ya nchi Wanachama wa *SADC. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuwawezesha wanawake kupanua uelewa wao kibiashara, wanawake 127 walishiriki maonyesho ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam kwa kuwezeshwa na Serikali ikishirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa wote *(Equal Opportunities Trust Fund – EOTF)* mwaka 2005, ikilinganishwa na wanawake 130 mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya takwimu zilizochambuliwa kijinsia katika maamuzi mbalimbali pamoja na kuhuisha sheria zinazoendelea kuwakandamiza wanawake. Serikali itahakikisha kiwango cha uwakilishi wa wanawake katika ngazi mbalimbali kinazingatiwa pamoja na kuhakikisha kuwa wanawake wanaendelea kupewa fursa ya kujiendeleza kielimu na kiuchumi ili waweze kufaidika zaidi katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya idadi ya watu Tanzania kwa kutumia takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, yanaonyesha kwamba kwa mwaka 2005 idadi ya watu ilikuwa 37,267,530 kati ya hao, wanawake ni 19,009,051, sawa na asilimia 51.01 na wanaume 18,258,479 sawa na asilimia 48.99. Tanzania Bara inakadiriwa kuwa na watu 36,197,313 wakati Tanzania Zanzibar ilikadiriwa kuwa na watu 1,070,217.

Mheshimiwa Spika, kutokana na makadirio hayo Mkoa wa Dar es Salaam, ulionyesha kuwa na msongamano wa *(density)* wastani wa watu 2,010 kwa kilomita ya mraba, ukifuatiwa na Mwanza watu 163 na Kilimanjaro watu 108. Mikoa iliyo na msongamano mdogo ilionyesha kuwa ni Lindi yenye watu 12 kwa kilomita ya mraba

ikifuatiwa na Rukwa watu 18 kwa kilomita ya mraba, ikifuatiwa na Rukwa watu 18. Kwa Tanzania Zanzibar karibu Mikoa yote ina msongamano mkubwa wa kati ya watu 117 na 1,919 katika kilomita ya mraba.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya idadi ya watu ilikamilika kuhuishwa katika mwaka 2005 na mpango wa utekelezaji ulianza kuandaliwa. Mafunzo ya namna ya kujumuisha masuala ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo yaliendelea kutolewa katika ngazi za Wilaya na Kata, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 Serikali iliandaa mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji. Mkakati umelenga kukabiliana na tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira utokanao na shughuli za ufugaji na kilimo kwenye maeneo ya vyanzo vya maji. Pia, mkakati huu unalenga kukabiliana na uharibifu wa mazingira utokanao na ukataji miti ovyo kwa ajili ya kuni, mkaa na matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 Serikali inategemea kuchukua hatua zifuatazo:-

Kudhibiti shughuli za kilimo na ufugaji kwenye vyanzo vya maji, kuendelea kuhamasisha wafugaji kuondokana na ufugaji holela na kuhamahama, kuandaa mipango mizuri ya matumizi ya ardhi, kuendeleza kampeni ya kitaifa ya upandaji miti na dhamana ya ardhi ambazo zilianza kutumika mwezi Agosti, 2005 na Sheria ya Kusajili shughuli za biashara ya mwaka 2006 na kutayarisha rasimu za Miswada kwa ajili ya sheria mbalimbali kama vile Miswada ya kuthamanisha ardhi, usalama kazini, fidia kwa wafanyakazi, hifadhi ya jamii na Uwakala wa Soko la Ardhi ambayo imekwishawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuwezesha maandalizi ya mkakati wa kuendelea sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Serikali itaendelea kuratibu MKUBITA kwa kutoa msukumo wa pekee na thabiti katika kuendeleza sekta binafsi kwa kuweka mazingira bora ya kufanyia biashara na uwezeshaji nchini hususan kuendelea kuboresha sera, sheria na taratibu zinazokwaza sekta binafsi kubadilisha mtazamo wa Watendaji wa Serikali kwa sekta binafsi, kuimarisha kituo cha uwekezaji wa Taifa na kuleta mageuzi katika Mahakama ya Biashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005 Serikali ilianza kutekeleza Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania *(Tanzania Mini-tiger Plan 2020)* kwa kuzingatia uzoefu na mafanikio ya nchi za Kusini Mashariki mwa Asia. Lengo la mpango huu ni kuongeza kasi ya ukuaji uchumi kama msingi wa kuongeza wastani wa kipato cha Mtanzania, kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nchi za nje na kuongeza fursa za ajira nchini kwa shabaha ya kukabiliana vizuri zaidi na tatizo la umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika harakati za kuendeleza Mpango huu, miradi ifuatayo ilitekelezwa; kuzinduliwa kwa kampuni ya kuagiza na kukarabati magari, mashine na vipuri mbalimbali *(Tsubasa Renewcar EA Limited)* na kuanza kwa ujenzi wa eneo

maalum la uwekezaji raslimali katika eneo la Mabibo Dar es Salaam linalojulikana kama "*The Benjamin William Mkapa Special Economic Zone (BWM-SEZ)*". Vilevile, Kamati ya kusimamia ujenzi wa Kituo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT -SEZ)* iliundwa na iliendelea na kazi zake chini ya uratibu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Aidha, Wataalam walitembelea India Oktoba 2005, ili kupata uzoefu wa kuanzisha na kuendesha vituo vya aina hiyo hapa nchini. Katika kufanikisha Mpango huu, Sheria ya kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji raslimali *(SEZs)* imepitishwa na Bunge lako Tukufu Februari, 2006 na kupata kibali cha Rais Machi, 2006 na kuanza kutumika rasmi tarehe 01 Mei, 2006.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, mpango huu utakuwa na malengo yafuatayo:-

Kuendelea na ujenzi wa kulitangaza eneo maalum la uwekezaji la '*Benjamin William Mkapa Special Economic Zone*' lililoko Mabibo ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi; kuunda mamlaka ya kusimamia maeneo maalum ya uwekezaji *(SEZs Authority);* kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Watanzania kutoka nchi zenye uzoefu wa maeneo maalum ya uwekezaji na kuanza ujenzi wa Kituo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Eneo Maalum la Uwekezaji lililoko eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(ICT-SEZ).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006, awamu ya kwanza ya MKURABITA ilihusu tathmini ya sekta isiyo rasmi na taarifa yake kukabidhiwa Serikalini tarehe 05 Oktoba 2005. Tathmini ilibainisha mtandao, thamani ya sekta isiyo rasmi, kanuni na taratibu zinazotumiwa na wadau kumiliki mali na kufanya biashara nje ya mfumo rasmi wa Sheria. Vile vile, tathmini iliainisha vikwazo vya kisheria vinavyowazuia Watanzania walio wengi kuzingatia sheria kikamilifu wafanyapo biashara na katika kumiliki mali hususani ardhi na majengo.

Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na uhamasishaji wa viongozi katika ngazi mbalimbali juu ya malengo na madhumuni ya MKURABITA; uhamasishaji kwa walengwa na watendaji kupitia warsha mbalimbali, uhamasishaji wa wafanyabiashara ndogondogo na za kati juu ya shughuli za MKURABITA; uandaaji wa taratibu za ushirikiano na Wizara na Taasisi za Serikali zinazoweza kufanya shughuli kwa ushirikiano na MKURABITA na ukamilishaji wa Mpango wa Kazi kwa ajili ya Awamu ya Pili ya MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, malengo ya MKURABITA ni pamoja na kufanya utafiti katika Wilaya 26 za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ili kuandaa mapendekezo ya awali ya maboresho ya Sheria na Kanuni zitumikazo katika sekta isiyo rasmi; kutoa mapandekezo ya awali ya muundo wa kitaasisi (*institutional arrangement);* kutoa mafunzo kwa wataalamu wa Kitanzania ili kuhakikisha umiliki na ushiriki wa Watanzania katika kutengeneza sheria; kutekeleza shughuli zinazokwenda sambamba na maandalizi ya maboresho ili kuendeleza nguvu na msukumo wa Watanzania ulitokana na taarifa ya utafiti; na kukamilisha *Concept Document* ya

programu ambayo itatumika kama kiongozi cha mpango huu na kuendeleza utengenezaji wa tovuti ya MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika awamu ya kwanza ya *TASAF* Serikali iliamua kuendelea na awamu ya pili ya *TASAF*. Utekelezaji wa *TASAF* umetokana na kupata mkopo wa gharama nafuu kutoka Benki ya Dunia wa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 129 na ruzuku ya Dola za Kimarekani milioni 21. Fedha hizo zimelenga kufanikisha malengo ya maendeleo ya milenia na ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Pili ya *TASAF* kilichoanza Mei 11, 2005, Serikali imefanikiwa katika kuhamasisha Umma kupitia vipindi vya radio na televisheni, makala katika magazeti na vipeperushi, kuandaa miongozo ya utekelezaji wa mradi katika ngazi za Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Jiji na Sheria na kutafsiri katika Lugha ya Kiswahili miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 , *TASAF* imejiwekea lengo la kuwafikia wananchi wote wa Tanzania kwa kutoa mafunzo kuhusu taratibu za utekelezaji wa miradi itakayofadhiliwa na *TASAF*.

Aidha, uratatibu utawekwa kuhakikisha kwamba wananchi wanatekeleza miradi kwa ufanisi, kusimamia kwa karibu utekelezaji na kuhakikisha kwamba taarifa za utekelezaji zinatolewa kwa wakati kwa ajili ya tathmini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Serikali kwa kupitia Baraza la Taifa la Biashara (*TNBC*) imeanza mabaraza ya biashara ya Mikoa kwa lengo la kupanua wigo wa mashauriano kati ya Serikali na Sekta Binafsi ili kuboresha mazingira ya uzalishaji na biashara katika Mikoa na Wilaya. Mabaraza hayo yameanzishwa katika Mikoa 12 ifuatayo:- Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga, Kagera, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Mtwara na Dodoma. Aidha, Baraza la Biashara la Zanzibar limeanzishwa chini ya Uenyekiti wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* iliendelea na juhudi za kuhamasisha na kuratibu wawekezaji wa ndani na nje katika sekta mbalimbali kwa lengo la kukuza sekta binafsi.

Katika mwaka 2005 Kituo kiliandikisha miradi 550 yenye thamani ya Shilingi milioni 1,876,063 ambayo ilitoa fursa za ajira kwa watu 55,663 ikilinganishwa na miradi 454 yenye thamani ya Shilingi milioni 1,246,040 mwaka 2004. Aidha, *TIC* inatekeleza mikakati ya kuibua fursa za uwekezaji Mikoani. Ili kutimiza azma hiyo, tayari kituo kimefungua Ofisi katika Kanda ya Ziwa Mkoani Mwanza na Kanda ya Kaskazini Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, thamani ya uwekezaji wa mitaji ya kigeni ya moja kwa moja yaani *(FDIs)* ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 325 mwaka 2005, ikilinganishwa na

Dola za Kimarekani milioni 470 mwaka 2004 sawa na upungufu wa asilimia 31. Upungufu huu ulisababishwa hasa na kushuka kwa uwekezaji katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/07 malengo ya *TIC* ni pamoja na kufungua Ofisi katika Kanda ya Kusini, kuendelea kuhamasisha wawekezaji wa nje kwa mtindo wa *Investor Targeting* ili kuongeza mitaji ya moja kwa moja kuwasaidia wawekezaji wadogo na wa kati *(SMEs)*; kuandaa miradi inayouzika *(Bankable Projects)* na kusaidiana na Mikoa katika kuandaa na kuratibu warsha za uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 jumla ya Mashirika 11 yalibinafsishwa na mali 126 ziliuzwa na kufanya jumla ya Mashirika yaliyobinafsishwa kuwa 322 na mali za Mashirika kuwa 647 tangu zoezi hili lianze miaka 13 iliyopita. Mashirika hayo yaliyobinafsishwa kwa Watanzania na Wawekezaji kutoka Nje kwa utaratibu wa kuuza hisa, kuuza mali na kukodisha. Aidha, Tume ya Rais ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma iliongezewa muda wa miaka minne kuanzia Januari, 2004 hadi Desemba, 2007 ili kukamilisha ubinafsishaji wa Mashirika yaliyobaki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/07 Mashirika 36 yaliyobaki yataendelea na hatua mbalimbali za marekebisho, yakiwemo *TAZARA*, vitengo vya Kibiashara vya Mamlaka ya Bandari Tanzania (ukiondoa kitengo cha makontena ambacho kimeshakodishwa) na Shirika la Bima la Taifa. *PSRC* itafikia mwisho Desemba 2007, ambapo zoezi hili linatakiwa liwe limekamilika. Baada ya hapo, azma ya Serikali ni kubakiza Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini yaani *(Monitoring and Evaluation)* ya Mashirika yaliyobinasishwa na kuratibu shughuli za Mamlaka za Udhibiti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi; uwezeshaji wa Watanzania kiuchumi umekuwa moja ya ajenda ya muda mrefu katika Sera ya Taifa letu. Jitihada za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi zimekuwa zikifanywa na vyombo mbalimbali hata kabla ya Sera ya Uwezeshaji kuundwa. Bunge lako Tukufu lilishuhudia uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Juni, 2004 na kupitisha Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Novemba, 2004, ambayo ilianza kutumika rasmi Februari, 2005. Lengo kuu la Sera hii ni kuwawezesha wananchi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kutoa mwongozo wa jumla utakaohakikisha kwamba, wananchi wanapata fursa za kiuchumi katika sekta mbalimbali.

Aidha, Baraza la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi liliundwa na kuzinduliwa rasmi Novemba 2005. Vile vile, Mheshimiwa Rais alimteua Katibu wa Baraza la Uwezeshaji tarehe 3 Aprili, 2006 akiwa na dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sera za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Pamoja na kuteuliwa kwa Katibu wa Baraza shughuli za Sekretariati ya Baraza la Uwezeshaji zitaanza kutekelezwa rasmi mwaka huu wa fedha 2006/07 ambapo Shilingi milioni1.4 zimetengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza sera hii, kila sekta inawajibika kuendelea kubuni mikakati yake. Kufafanua na kuchanganua jinsi ya kuitekeleza. Mikakati ya kisekta inaendelea kujikita zaidi katika kuwaendeleza wananchi kwa kuwapa upendeleo

maalum na kuwawezesha kwa kuwapatia huduma bora za elimu na mafunzo ya ujasiriamali, kujenga miundombinu na kuwapa fursa za kushiriki katika kubuni, kupanga na kutekeleza sera na mikakati ya kisekta ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 baadhi ya kazi zitakazofanywa na Serikali ni kuajiri Watumishi wa Sekretariati ya Baraza, kufanya utafiti wa kuainisha mambo muhimu ya kipaumbele *(Quick wins)* katika kutekeleza Sera hii; kuandaa mwongozo wa jinsi wananchi watakavyoshiriki katika kutekeleza Sera; na kuandaa mfumo wa kuhakikisha kwamba sera ya uwezeshaji inafahamika vizuri zaidi kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, licha ya Tanzania kupata mafanikio makubwa katika uchumi jumla, changamoto kubwa iliyopo ni kuendeleza na kuhakikisha kwamba mafanikio hayo yanawafikia wananchi wengi, hususan wananchi maskini walio Vijijini. Aidha, kukamilika na kutekelezwa kwa kikamilifu miradi ya Vitambulisho vya Taifa; Upimaji na Utoaji Hatimiliki na Utayarishaji wa Ramani Maalum za Maeneo zinazosomeka kwa Kompyuta *(Geographical Information System – GIS and National Spatial Data Infrastructure – NSDI)* kutafanikisha kupatikana takwimu sahihi na katika muda muafaka. Takwimu hizi zitasaidia katika tafiti mbalimbali zinazohusu jamii na maendeleo.

Aidha, katika kuendeleza juhudi za kuwawezesha wananchi kiuchumi, Serikali imeanzisha mfuko wa dhamana kwa *SMEs* na inaendelea kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali iliyoanzishwa ikiwemo MKURABITA; MKUBITA; *Tanzania Mini Tiger 2020* na *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, misingi na malengo ya mpango wa muda wa kati na bajeti kwa mwaka 2006/2007 – 2008/2009. Mpango huu na Bajeti hii ni ya kwanza kutayarishwa na Serikali ya Awamu ya Nne katika kutekeleza MKUKUTA. Misingi na Malengo ya Mpango wa Muda wa Kati na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2006/2007 – 2008/2009 inazingatia utekelezaji wa ahadi ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, inayolenga katika kuyafikia malengo maku ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ikijumuisha kuwapo maisha bora ya kila Mtanzania na kupunguza kabisa umaskini wa kipato ifikapo 2015. *(Makofi)*

Mfumo wa Makadiri ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007 utatolewa na Waziri wa Fedha ambapo atabainisha kwa kina mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali katika mwaka 2005/06 na makadirio kwa mwaka 2006/2007 pamoja na kufafanua maeneo makuu yaliyotengewa fedha.

Mheshimiwa Spika, misingi ya malengo mapana ya Mpango wa Bajeti kwa kipindi cha muda wa kati 2006/2007 – 2008/2009 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kutengemaza uchumi mkuu au uchumi jumla *(Macro economic stability)*

(ii) Kuendelea kutekeleza MKUKUTA kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuendelea kutekeleza miradi mikubwa kama MKURABITA, Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo Tanzania, Mradi wa Maji kutoka Ziwa *Victoria* kwenda Kahama-Shinyanga, ujenzi wa barabara na madaraja pamoja na miundombinu ya umwagiliaji maji;

(iii) Kuendelea kubuni na kutekeleza mipango na mikakati ya kuharakisha ukuaji wa uchumi kwa mfano mradi wa Vitambulisho vya Taifa, mradi wa upimaji ardhi na utoaji hatimiliki na utayarishaji wa ramani maalum za maeneo zinazosomeka kwa kompyuta *(Geographical Information System – GIS and National Spatial Data Infrastructure-NSDI);*

(iv) Kuimarisha na kusaidia sekta isiyo rasmi ili ipanuke na kutengemaa kwa lengo la kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa uchumi;

(v) Kuimarisha mifumo ya uratibu na usimamizi wa miradi ya maendeleo katika ngazi zote;

(vi) Kuendelea kutekeleza sera za Serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi kupitia programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa;

(vii) Jamii kuwa na mwamko, nidhamu na tabia ya kujituma katika shughuli za maendeleo; na

(viii) Kupatikana kwa rasilimali na kuzitumia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia misingi niliyouitaja hapa juu, matarajio ya malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2006/07-2008/09 ni kama ifuatavyo:-

(i) Pato halisi la Taifa kukua kwa asilimia 5.9 mwaka 2006, asilimia 7.3 mwaka 2007, asilimia 7.7 mwaka 2008 na asilimia 7.9 mwaka 2009;

(ii) Kiwango cha kasi ya upandaji bei kisichozidi asilimia 4.0 (kwa bei za 2001) kufikiwa ifikapo mwezi Juni 2007;

(iii) Mapato ya ndani kuongezeka kufikia asilimia 14.5 ya Pato la Taifa katika mwaka 2006/07, asilimia 14.7 mwaka 2007/08 na kuongezeka hadi asilimia 14.7 mwaka 2007/08 na kuongezeka hadi asilimia 14.8 mwaka 2008/09;

(iv) Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana, (M2) kudhibitiwa kwa viwango vinavyowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei; na

(v) Akiba ya fedha za kigeni itakayokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi saba.

Mheshimiwa Spika, majumuisho, baada ya kuelezea hali ya uchumi wa Taifa, misingi na malengo ya mpango na bajeti kwa kipindi cha 2006/2007-2008/2009, nachukua fursa hii kusisitiza mambo muhimu ambayo kama Taifa tunahitaji kuyapa kipaumbele katika utekelezaji na ufuatiliaji wa karibu kwa mwaka 2006/07 kama ifuatavyo:-

(i) Kuhakikisha kwamba wananchi wanaelewa masuala muhimu yote yaliyobainishwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 na Mkakati wa Kukuza uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, kupitia vyombo mbalimbali vikiwemo Televisioni, Radio, Tovuti ya Taifa na magazeti mbalimbali;

(ii) Kuendelea kuhakikisha kwamba mipango, mikakati na malengo tunayojiwekea yanalenga katika kukuza uchumi, kuongeza nafasi za ajira, kuongeza tija na kuongeza mapato ya fedha za kigeni na ya ndani;

(iii) Kuendelea kukasimu baadhi ya madaraka ya Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa pamoja na kuzipatia rasilimali kwa lengo la kuwapa wananchi uwezo wa kuchambua, kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathimini mipango na mikakati yao inayolenga katika kuwaondolea umaskini;

(iv) Kuendelea kuboresha na kuoanisha mifumo ya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa mipango na mikakati ya maendeleo kama ilivyoainishwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 na malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2025 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania yaani MKUKUTA;

(v) Kuendelea kuhamasisha Sekta zote zibuni mikakati madhubuti na endelevu ili kuboresha hali ya maisha ya wananchi wetu;

(vi) Kuendelea kuboresha na kurasimisha Sekta isiyo rasmi ili ipate kupanuka na kutengemaa kwa lengo la kuongeza nafasi za ajira nchini;

(vii) Kuendelea kuhimiza wawekezaji wa ndani kuwekeza katika viwanda vidogo na vya kati vya kusindika mazao ya kilimo ili kuongeza thamani yake na kuchangia katika kupanua nafasi za ajira;

(viii) Kuendelea kubuni na kutekeleza mipango na mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ili waweze kuboresha na kuendeleza shughuli zao za kijamii na kiuchumi; na mwisho

(ix) Kuendelea kuhuisha mikakati ya Kitaifa ya kujitosheleza kwa chakula kwa lengo la kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 hatuna budi kulinda mafanikio yaliyopatikana wakati wa Serikali ya Awamu ya Tatu na kulenga katika kuendelea kupata mafanikio zaidi kwa nia ya kuondoa kero zinazowasibu wananchi walio wengi. Katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Nne hatuna budi kuwa makini zaidi katika kubainisha vipaumbele vyetu vya kukuza uchumi na kuondoa umaskini.

Kwa hiyo, kwa kutambua kwamba rasilimali zetu ni finyu ni lazima tuelekeze rasilimali za kutosha katika maeneo machache yatakayochochea maendeleo yetu kwa haraka zaidi uamuzi ambao utafanya tuahirishe shughuli nyingine au kuzipa rasilimali chache za kukidhi gharama za uendeshaji tu. Changamoto tuliyonayo ni kukubaliana ni maeneo gani yapewe kipaumbele zaidi katika mgao wa rasilimali na pia kuheshimu maamuzi hayo. Aidha, ili kuongeza ufanisi zaidi katika utekelezaji wa sera, mipango na mikakati yetu kuna haja ya kuboresha mifumo ya kutekeleza na kuendelea kusimamia, kufuatilia na kutathimini malengo kwa makini zaidi ili uchumi wa Taifa letu ukue kwa haraka zaidi ili uchumi wa Taifa letu ukue kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelezea kuwa rasilimali zetu bado ni kidogo ukilinganisha na matatizo mengi ya kijamii na kiuchumi yanayotukabili Kitaifa. Tunaweza kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii kwa haraka zaidi ikiwa tutatumia rasilimali tulizonazo kwa ufanisi na makini zaidi. Hivyo, wito wangu ni kwa kila mmoja wetu kutumia fursa zilizopo kwa lengo la kuongeza tija kwa kasi kubwa na kukuza uchumi wetu kwa nguvu zaidi ili tuondokane na umaskini uliokithiri.Aidha, ni lazima jamii iwajibike kudhibiti, kufuatilia, kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mipango na mikakati na kutathimini malengo. Serikali itaendelea na jukumu la kuwawezesha na kuunga mkono juhudi za wananchi kwa kuelekeza rasilimali, pamoja na kuendelea kuandaa sera na mikakati na kutoa miongozo ya kuratibu, kusimamia pamoja na kufuatilia kwa karibu na kutathmini utekelezaji ili tuwe na maendeleo yenye kuwiana katika kila ngazi. Hivyo basi, kila mmoja wetu anatakiwa kutimiza wajibu wake ili kufikia azma ya Taifa ya ukuaji wa uchumi unaopanda mwaka hadi mwaka na kwa haraka zaidi ili kufikia malengo ya MKUKUTA na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nitambue juhudi za washirika mbalimbali wa maendeleo yetu kwa misaada na michango yao ambayo imekuwa chachu kwa maendeleo yetu. Naomba sasa nitumie fursa hii kuwashukuru wote waliotusaidia na kutoa pongezi zetu za dhati kwa kuzitaja nchi hizo, Taasisi na Mashirika kama ifuatavyo:-

Serikali za Uswisi, Uholanzi, Ujerumani, Denmark, Ufaransa, Uingereza, Hispania, Ubelgiji, Canada, China, Afrika ya Kusini, Japan, Kuwait, Italia, Ireland na nchi nyingine marafiki. Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)*, Mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa kama vile *UNDP, UNESCO, UNFPA, UNHCR, UNICEF, UNIFEM, FAO, IFAD, WFP na WHO*, Jumuiya ya nchi za Ulaya (EU), Mfuko wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Uzalishaji Mafuta *(OPEC FUND)*, Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Uingereza Shirika la Maendeleo la Norway *(NORAD)*,

Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID),* Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA),* Shirika la Maendeleo la Finland *(FINNIDA*), Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA),* Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)*, Shirika la Maendeleo ya Uswisi *(SDC),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali *(NGO's). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa na iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangulia kusema hoja hiyo imekwishatolewa, lakini kwa utaratibu wetu itaamuliwa wiki ijayo. Naomba kutangaza tu kwamba hadi sasa nimepata majina ya wachangiaji ya Waheshimiwa Wabunge 51. Niseme tu, kwa sababu ni siku tano, basi bado tunapokea maombi ya wale wanaotaka kuchangia.

Kuna matangazo machache. Kutakuwa na Kikao cha dharura cha Wajumbe wa Kamati ya Utendaji *(Executive Committee)* ya *APNAC* kesho Ijumaa tarehe 16 Juni, 2006 saa 4 kamili, Ukumbi Na. 219 Jengo la Utawala, Ghorofa ya pili. *APNAC Executive Committee* saa 4.00 asubuhi kesho Chumba Namba 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Mohamed Missanga, anawatangazia Wajumbe wake wote wa Kamati ya Miundombinu kuwa kuna Kikao muhimu sana saa 3.30 Ukumbi Namba 231 ambapo watakutana na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu. Kamati ya Miundombinu saa 3.30 asubuhi kesho ghorofa ya pili Chumba Namba 231.

Wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *LAAC* pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala wanaarifiwa kwamba saa 2.00 asubuhi kesho na kwa siku mbili 16/6/2006 na 17/6/2006 kutakuwa na Semina itakayoendeshwa na Wataalam kutoka Kitengo cha Mpango wa Uboreshaji wa Serikali za Mitaa TAMISEMI. Semina hiyo itafanyika *Dodoma Hotel.* Inatazamiwa kufunguliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa. Kwa hiyo, saa 2.00 kesho *Dodoma Hotel* Semina ya Maboresho na Uboreshaji wa Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wajumbe wote wa Kamati hizo mbili *LAAC* na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wahudhurie bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge wote ambao wana shughuli na Kampuni ya *TOYOTA Tanzania* wabakie kwa dakika tano baada ya kusitisha shughuli. Waheshimiwa Wabunge nimepokea malalamiko mengi kuhusu kupekuliwa pale getini. Inaelekea utaratibu unakuwa mzito sana. Lakini tutajaribu kushauriana na Idara zinazohusika ili tuone njia zipi zinaweza kurahisisha kidogo matatizo ya ndani.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu mambo haya ya taa ndani ya Ukumbi huu, nimeandikiwa pia na wanaohusika na upigaji picha humu ndani kwamba inapokuwa giza, sasa hata nyuso zenu hazitaonekana. Lakini napenda kusoma maoni ya Mheshimiwa mmoja ambaye wala hakujitaja lakini nayaona mazuri tu. Anasema hivi:-

"Mheshimiwa Spika, utapata shida sana mara taa kali, mara giza. Hawa Waheshimiwa wenzetu wanaolalamika badala ya kusikiliza na kusoma nyaraka zao, macho yao yako juu tu kuangalia taa nzuri. Ndiyo maana macho yao yanapata shida wakifanya kazi zao za kibunge kama zinavyotakiwa, hakuna haja ya kuangalia juu kila wakati.*(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uliangalie hili la sivyo watakuchanganya. Hakuna taa kali, bali wasiangalie taa huko juu. Wanatamani kuona mandhari ya juu, ndiyo tatizo. Wala wewe na Katibu msiumize vichwa vyenu, la sivyo mtaambiwa kila kitu humu ndani ya Ukumbi wa Bune mbadili." *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sasa hivi naona niupokee ushauri huu kwa sababu sio vizuri Waheshimiwa Wabunge msionekane katika picha, inaua kabisa makusudi na pia wale ambao wanasema kuhangaika kuhusu taa, nashukuru ushauri huu. Taa hizo zitakuumiza tu ukiwa unang'ang'ania kuziangalia. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, la mwisho, naomba niwasomee mawili tu ambayo nimeyapata. Huwa napenda muwe na mimi kwa sababu mtaona nayafanyia kazi vipi. Mbunge mmoja ambaye anakaa upande wa kulia huku, amesema:- "Mheshimiwa Bwana Spika, salaam. Inaelekea jicho la Spika linaelekea mkono wa kushoto zaidi. Je, Kanuni ipi itumike ili jicho la Spika la mkono wa kuume nalo liwe na huruma hasa kwa Wabunge wanaokaa mkono wa kulia?" *(Makofi)*

Baada ya kuipata hiyo, nikaipata ya pili. "Mheshimiwa Spika, shikamoo kaka. Tunaomba uwe pia unaangalia upande wa kushoto. Mimi nimekuwa nikitafuta kuuliza swali kuhusu mambo ya mpakani lakini hunioni. Natanguliza shukrani zangu."

Waheshimiwa Wabunge, ni dhahiri kama Spika angekuwa haangalii kushoto wala kulia kusingekuwa hata na maswali. Kwa hiyo, naamini kabisa Spika anatenda haki na kwa hiyo ni matatizo tu, siku nyingine unaweza kudhani ni hivyo lakini sivyo. Kwa hiyo, nawahakikishia kabisa najitahidi kabisa kutenda haki pamoja na Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti. Kwa hiyo, hakuna ukweli kwamba napendelea kushoto wala kulia.

Baada ya kusema hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 10 leo jioni .

*(Saa 05.54 asubuhi Bunge lilisimamishwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2006/2007

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Pamoja na hotuba hii, vimetayarishwa vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina takwimu za Bajeti. Kitabu cha kwanza kinahusu Makisio ya Mapato. Kitabu cha Pili na cha Tatu vina Makisio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri za Miji na Wilaya. Kitabu cha Nne, kinaelezea Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara na Mikoa pamoja na Halmashauri. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2006/2007 ambao ni sehemu ya Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kupitia Chama cha Mapinduzi kwa kura nyingi kuwa Rais wa Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu nchi yetu kupata Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nampongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Rais na baadaye kuthibitishwa na Bunge letu kwa kura nyingi kuwa Waziri Mkuu. Nakupongeza wewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuongoza Bunge letu. Nawapongeza nyote Waheshimiwa Wabunge kwa kuchaguliwa katika Majimbo yenu na wengine kuwakilisha jumuiya zenu kupitia Viti Maalum. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kuongoza Wizara zenu. Sote tuna dhamana kubwa ya kuwahudumia wananchi na kukidhi matumaini yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sasa binafsi kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais, kwanza, kwa kuniteua kuwa Mbunge na kisha Waziri wa Fedha wa kwanza mwanamke. Mheshimiwa Rais amenipa heshima kubwa na napenda kumhakikishia yeye, Chama changu na wananchi wote kwa ujumla kuwa nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote na ninamwomba Mwenyezi Mungu anisaidie. *Amina. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya Bajeti hii ambayo maandalizi yake yamehusisha wadau wengi. Napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuchambua Makisio yote ya Mapato na Matumizi. Ushauri wa Kamati hii umesaidia sana kuboresha Bajeti ninayowasilisha leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Wizara zote, Idara zinazojitegemea, Mikoa, Halmashauri za Miji na Wilaya, Taasisi za Kitaifa na Kimataifa na wawakilishi wa sekta binafsi, kwa michango yao iliyosaidia kufanikisha Bajeti hii.

Naomba niishukuru kwa namna ya pekee ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha na nyaraka mbalimbali za Sheria kama sehemu ya Bajeti hii. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Fedha nikianza na Naibu Mawaziri wa Fedha, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Katibu Mkuu, Ndugu Gray Mgonja, Naibu Makatibu Wakuu, Ndugu Ramadhan Khijjah na Ndugu Joyce Mapunjo, Wakuu wa Idara, na wafanyakazi wote wa Hazina. Namshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii, vitabu vya Bajeti, pamoja na nyaraka nyingine zinazohusu Bajeti hii kwa wakati.

Mwisho, nawashukuru kipekee wataalam na wale wote waliotoa mapendekezo kuhusu maboresho ya ukusanyaji wa kodi mbalimbali. Mapendekezo na ushauri wao umezingatiwa katika kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu wa Bajeti ni wa kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika mwezi Desemba, 2005. Katika uchaguzi huo, Chama cha Mapinduzi kilipata kwa kishindo kikubwa ridhaa ya wananchi ya kuendelea kuiongoza nchi yetu. Ushindi huo wa CCM ulidhihirisha siyo tu imani kubwa waliyo nayo wananchi kwa Chama cha Mapinduzi, bali pia matarajio na kiu yao ya maendeleo kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati akifungua Bunge hili tarehe 30 Desemba, 2005, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alieleza bayana majukumu ya msingi ya Serikali ya Awamu ya Nne kwamba ni pamoja na, nanukuu:“Kwanza, kuitoa Tanzania kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa uchumi wa kisasa wa Tanzania linalojitegemea na pili, kuwashirikisha wananchi wote kwa njia ya uwekezaji katika ukuzaji wa uchumi na kutokomeza umaskini.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ni mwanzo wa kutekeleza mikakati ya kufikia malengo hayo aliyoyaeleza Mheshimiwa Rais. Katika kutafakari na kuchangia Bajeti hii ya mwaka 2006/2007, hatuna budi kuzingatia lengo kuu la kukuza uchumi kwa kasi zaidi na kuwajumuisha wananchi walio wengi zaidi kushiriki na pia kufaidika na matunda ya uchumi imara.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa sera za Bajeti ya mwaka 2005/2006, mwenendo wa viashiria muhimu vya uchumi kwa kipindi cha Julai, 2005 hadi Machi, 2006 ulikuwa wa kuridhisha licha ya janga la ukame ambalo lilisababisha uhaba mkubwa wa chakula na upungufu mkubwa wa maji kwa ajili ya kuendesha mitambo inayozalisha umeme. Aidha, kupanda mfululizo kwa bei ya mafuta ya petroli katika soko la dunia kumeongeza gharama za uzalishaji na huduma mbalimbali. Matukio haya yalisababisha mfumuko wa bei nchini kupanda kutoka asilimia 4.3 mwisho wa Julai, 2005 hadi asilimia 6.9 mwezi Aprili, 2006. Hata hivyo, kama alivyoelezea Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, uchumi umekua kwa asilimia 6.8 mwaka 2005 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2004. Vile vile, akiba

ya fedha za kigeni kwa mwaka 2005 ilikuwa inatosha kulipia bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi 6.4.

Tathimini inaonyesha kwamba utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2005/2006 kwa miezi sita ya mwanzo ya mwaka wa fedha umekuwa wa kuridhisha licha ya madhara ya ukame na kupanda kwa bei ya mafuta.

Hata hivyo, upungufu wa chakula ulilazimu Serikali kufanya marekebisho ya ndani kwa ndani katika Bajeti yake ili kununua na kusambaza chakula cha njaa kwa wananchi wa maeneo yaliyoathirika zaidi na uhaba huo na pia kununua umeme wa *IPTL* na *Songas*. Hatua nyingine ni pamoja na Serikali kutoa msamaha wa kodi kwa nafaka kutoka nje ya nchi ili chakula kipatikane kwa wingi na kwa bei nafuu kwa walaji. Kwa pamoja, hatua hizi zilipunguza makali ya uhaba wa chakula na kuokoa maisha ya wananchi wengi. Hatua hizi zilisaidia pia kuzuia mfumuko wa bei usipande sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2005/2006, Serikali ililenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi trilioni 2, bilioni 66, milioni 751 (shilingi 2,066,751milioni). Ili kuboresha ukusanyaji wa mapato, hatua kadhaa zilichukuliwa ambazo ni pamoja na kuimarisha utendaji na usimamizi katika Idara ya Forodha, kurekebisha muundo wa Mamlaka ya Mapato ili kuboresha zaidi usimamizi wa vyanzo vya ndani vya mapato, kuimarisha idara ya walipakodi wakubwa ili ihudumie walipakodi wengi zaidi na kwa kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi katika maeneo kadhaa ili kurahisisha ukusanyaji na ufanisi wa usimamizi wa kodi. Hadi mwezi Machi, 2006 jumla ya shilingi trilioni 1, bilioni 544, milioni 366 (shilingi 1,544,366 milioni) zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 100.5 ya lengo la kipindi hicho. Mwelekeo unaonyesha kwamba lengo la mapato kwa mwaka 2005/2006 litafikiwa. Yafuatayo ni maelezo ya baadhi ya hatua zilizochukuliwa katika mwaka wa 2005/2006 kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali:-

(i) Marekebisho ya Kodi ya Mapato, Serikali ilirekebisha viwango vya kodi ya mapato yatokanayo na ajira (*PAYE*) katika Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, kwa kuongeza kiwango cha chini cha mapato ya ajira yasiyotozwa kodi, kutoka shilingi 60,000 kwa mwezi hadi shilingi 80,000 kwa mwezi. Hatua hii ilitoa unafuu wa kodi kwa wafanyakazi wa kipato cha chini kwa kuwaondoa katika wigo wa kodi.

(ii) Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa sura namba 147, viwango vya Ushuru wa Bidhaa kwenye vinywaji baridi, bia, mvinyo kutoka nje ya nchi, vinywaji vikali na sigara viliongezwa kwa asilimia 5 ili kwenda sambamba na mfumuko wa bei. Mapato yaliyokusanywa kutokana na kianzio hiki katika miezi tisa ya Julai, 2005 hadi Machi, 2006 yaliongezeka kwa asilimia 16.5.

(iii) Marekebisho ya Mfumo wa Kodi ya Ongezeko la Thamani yaani *VAT*, Serikali ilifanya marekebisho katika Sheria ya *VAT* sura namba 148 kwa nia ya kutoa unafuu ya ukwepaji kodi. Marekebisho hayo ni pamoja na kutoa msamaha wa *VAT* kwa vipuri vya treni na vifaa vingine vinavyotumika katika treni ili kupunguza gharama za

usafirishaji na kusaidia Mashirika yetu ya reli yaani *TRC* na *TAZARA*, kumudu gharama za matengenezo. Serikali pia ilitoa msamaha kwa magari maalum ya kutoa huduma za afya (*Mobile Health Clinics)* ili kuvutia huduma hizo katika maeneo yasiyo na Vituo vya Afya au Zahanati. Hali kadhalika, Serikali ilitoa msamaha wa kodi kwa mafuta ya ndege ili kuziwezesha kampuni za ndege za hapa nchini kuhimili ushindani, kutokana na ongezeko kubwa la gharama za kuendesha ndege.

(iv) Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Ushuru wa Forodha, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilianza kutekeleza mfumo wa viwango vya Ushuru wa Forodha wa pamoja mwezi Januari, 2005. Katika kipindi cha Julai, 2005 hadi Machi, 2006, mapato kutokana na Ushuru wa Forodha yalikuwa asilimia 52 zaidi ya mapato ya kipindi kama hicho mwaka wa fedha wa 2004/2005. Huu ni uthibitisho kwamba Tanzania ilifanikiwa kulinda mapato yake ipasavyo wakati wa majadiliano ya kuanzisha Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(v) Mheshimiwa Spika, marekebisho ya Mfumo wa Leseni za Biashara, hatua zilizotekelezwa katika eneo hili ni kufanya marekebisho ya viwango vya baadhi ya ada zinazotozwa na vyombo mbalimbali ili kuboresha mazingiara ya biashara na uwekezaji. Hatua hizi ni pamoja na kufuta ada za leseni za usafirishaji zinazotozwa na mamlaka mbalimbali kwa magari yasiyochukua abiria kama vile magari ya mizigo madogo na makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2005 hadi Machi, 2006, misaada na mikopo ya nje ya masharti nafuu ilifikia shilingi trilioni 1, bilioni 364, milioni 244 (shilingi 1,364,244 milioni) ikilinganishwa na Makadirio ya shilingi trilioni 1, bilioni 443, milioni 580 (Shilingi 1, 443,580 milioni) katika kipindi hicho. Kati ya hizo, misaada na mikopo inayopitia kwenye Bajeti ya Serikali ilifikia jumla ya shilingi bilioni 575, milioni 956 ikilinganishwa na makisio ya shilingi 589,913 milioni (shilingi bilioni 589, milioni 913). Mikopo na misaada ya miradi ya maendeleo ilifikia shilingi 731,711 milioni (shilingi bilioni 731, milioni 711 milioni (shilingi bilioni 783 milioni 467) zilizotegemewa awali. Misaada na Mikopo ya nje haikufikia lengo katika kipindi hicho kutokana na sababu mbalimbali. Sababu kubwa ni, kwamba baadhi ya nchi wahisani zilikuwa na chaguzi ambazo zilibadilisha Serikali na hivyo kukawa na ucheleweshaji wa kutoa misaada iliyoahidiwa.

Mheshimiwa Spika, Mapato kutokana na ubinafsishaji yalifikia shilingi bilioni 33,309 ikilinganishwa na Makisio ya shilingi bilioni 5, milioni 210 (shilingi 5,210 milioni) kutokana na mauzo ya hisa za Serikali katika Benki ya *NMB*.

Mheshimiwa Spika, hadi mwisho wa Machi, 2006, Matumizi yote yalifikia shilingi trilioni 3, bilioni 180, milioni 542 (shilingi 3,180,542 milioni) karibu sawa na Makisio ya shilingi trilioni 3, bilioni 171, milioni 84 (shilingi 3,171,084 milioni) katika kipindi hicho. Matumizi ya kawaida yalifikia shilingi trilioni 2, bilioni 199, milioni 632, na matumizi ya miradi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 980, milioni 911. Malipo ya madeni na pensheni yalitumia shilingi bilioni 440, milioni 623 na mishahara ilitumia shilingi bilioni 486, milioni 511 (shilingi 486,511 milioni). Malipo ya pensheni ni pamoja

na madai ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ilivunjikwa mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi bado unaendelea kwa wale wanaojitokeza na madai hasa wale wa mirathi. Inatarajiwa kwamba zoezi hili litakamilika ifikapo mwishoni wa Juni, 2006. Kama watakuwepo wadai watakaosalia, malipo yao yataendelea kushughulikiwa katika mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika kipindi cha Julai, 2005 hadi Machi, 2006, Serikali inaamini kwamba lengo la Mapato la mwaka wa 2005/2006 litafikiwa bila shaka yoyote. Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia trilioni 2, bilioni 6, milioni 751 sawa na asilimia 14.3 ya Pato la Taifa kwa mujibu wa takwimu za Pato la Taifa zilizokuwepo. Hata hivyo, kwa kuzingatia marekebisho ambayo yamefanywa hivi karibuni ya takwimu za Pato la Taifa zilizotolewa na Wakala wa Takwimu, uwiano huu unakua asilimia 13.6 badala ya 14.3. Malengo ya misaada na mikopo kutoka nje ikijumuisha misamaha ya madeni, pia yatafikiwa. Kwa upande wa Matumizi, mwelekeo unaonyesha kwamba matumizi ya kawaida yatakuwa kama yalivyopangwa baada ya marekebisho kutokana na uhamisho wa ndani kukidhi mahitaji mbalimbali ya dharura yaliyotokana na sababu nilizoeleeza awali. Aidha, matumizi ya maendeleo yanategemewa kuwa kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wananchi kiuchumi katika mwaka wa 2005/2006, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya soko la fedha na la mitaji. Miswada ya Sheria mpya ya Benki kuu ya mwaka 2006 na Sheria ya Mabenki na Asasi za Fedha ya mwaka 2006, iliwasilishwa Bungeni na kupitishwa mwezi Aprili, 2006. Moja ya malengo muhimu ya sheria hizo ni kuipa Benki Kuu uwezo na uhuru zaidi wa kusimamia kikamilifu benki na taasisi za fedha nchini ili kupanua huduma za sekta hiyo, hasa kuwezesha wananchi kupata mikopo ya masharti nafuu ili washiriki kikamilifu kujiondolea umaskini. Ikumbukwe kwamba sekta ya fedha imara ni nguzo muhimu ya uchumi imara na inapaswa kutoa mchango wake katika kuwezesha wananchi kupata mikopo hasa ya uzalishaji. Marekebisho hayo ya sheria ni sehemu ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mpango wa Uboreshaji wa Sekta ya Benki. Maeneo muhimu ya Mpango huo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha mazingira ya kisera na sheria ili kuwezesha sekta ya benki kukua zaidi ili huduma ya benki iwafikie wananchi walio wengi;

(ii) Kuimarisha masoko ya fedha ili kuongeza ushindani wa tija;

(iii) Kuboresha usimamizi wa Mifuko ya Mafao ya Uzeeni;

(iv) Kuimarisha sekta ndogo ya bima;

(v) Kujenga mazingira ya upatikanaji wa huduma ya mikopo midogo midogo;

(vi) Kuwezesha ardhi kutumika kama dhamana kwa ajili ya mikopo; na

(vii) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kudhamini mikopo ya mabenki kwa wananchi kupitia Mfuko ya Dhamana ya Mikopo ya Mauzo ya Nje na Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa biashara ndogo ndogo. Mifuko hii inaratibiwa na Benki Kuu. Aidha, Serikali iko katika hatua za mwisho za kuanzisha rasmi Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya Maendeleo. Serikali inakiri kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi ya kutoridhishwa na utendaji wa mifuko hiyo ya dhamana iliyokwishaanzishwa. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 mifuko hiyo itafanyiwa tathimini ya kina na marekebisho yanayotakiwa yatafanywa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza Mpango wa Kurasimisha Biashara na Mali za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), ili kuzipa uhai kisheria rasilimali mfu zinazomilikiwa na kutumiwa na wananchi wa kawaida katika shughuli zao za kujikimu. Mpango huu unatambua ukubwa wa sekta isiyo rasmi, thamani ya mtaji mfu katika sekta hiyo, taratibu zake za kiutendaji na mchango mkubwa unaoweza kutolewa na sekta hii katika kukuza uchumi wa nchi. Mapendekezo ya jinsi ya kurasimisha sekta isiyo rasmi yanaandaliwa ili kutambua rasilimali za wananchi na kuwapa hati miliki zinazoweza kutumika, pamoja na mambo mengine, kama dhamana ya kukopa fedha kutoka benki kwa ajili ya kuboresha mitaji na maisha yao kwa ujumla.

Katika mwaka huu wa fedha, Serikali ilianza mchakato wa kuigeuza Benki ya Rasilimali (*TIB*) kuwa Benki ya Maendeleo ambayo itaratibu upatikanaji wa mikopo ya uwekezaji na uzalishaji wa sekta zote zikiwemo sekta za kilimo na viwanda. *TIB* imeongezewa mtaji kwa hatua ya mwanzo na sasa inajikita katika kuimarisha uwezo wa raslimali watu kabla ya kupanua shughuli zake. Aidha, Serikali inaboresha mazingira kuwezesha uanzishwaji wa vyombo vingine vya kuwapatia wananchi mitaji kwa ajili ya shughuli za uzalishaji kama nitakavyoeleza baadae katika Hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, changamoto zilizo mbele yetu, pamoja na mafanikio mengi ya kiuchumi na kijamii, nchi yetu bado inakabiliwa na changamoto nyingi, zikiwemo zifuatazo:-

(i) Kwanza, uwezo wa Serikali wa kutatua matatizo ya umaskini bado ni mdogo. Kwa hiyo, tunalo jukumu kubwa la kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuimarisha utawala wa kodi, kuiingiza sekta isiyo rasmi ndani ya wigo wa kodi, kuziba mianya ya ukwepaji wa kodi, kuimarisha masoko ya ndani ya kifedha ili kuwezesha wananchi kukopa na kupata mitaji ya kujiendeleza, na kuendelea kuboresha mazingira ya kuvutia uwekezaji, ambao ndio utapanua wigo wa kodi, na ajira.

(ii) Pili, sehemu kubwa ya mapato yetu ya fedha za kigeni inatokana na misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka nje. Mauzo ya bidhaa na huduma za Tanzania nje ya nchi ni kidogo sana. Hatuna budi kuweka nguvu mpya katika kukuza mauzo ya nje.

(iii) Kazi hii sharti ianze kwa kutambua na kufanyia kazi maeneo ambayo yanaweza kutupatia mafanikio kwa haraka na kutuongezea uwezo wa kiushindani katika soko la dunia.

(iv) Tatu, ni vyema tutumie misaada ya Wahisani kwa njia ambazo zinatusaidia kujenga uwezo wa nchi wa kujitegemea siku za usoni. Kwa sababu hiyo, maamuzi ya wapi misaada ielekezwe ni muhimu sana.

(v) Nne, ingawa nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali imekuwa bora kuliko huko nyuma, bado uko udhaifu katika kusimamia fedha za Serikali na hatua za kuondoa udhaifu huo zinachukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhusiano wetu na Wahisani, katika mwaka huu wa fedha, Serikali imeendelea kuboresha uhusiano wetu na nchi wahisani pamoja na mashirika ya fedha ya kimataifa chini ya mikakati tuliyojiwekea. Tumeendelea kupata misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Lengo kubwa la mikakati hii ni kuhakikisha kwamba Serikali ya Tanzania inamiliki *agenda* ya maendeleo ya nchi yetu badala ya wahisani, kuhakikisha misaada ya nje inapatikana na inaendelea kuongezeka na kwamba fedha nyingi zaidi zinapitia kwenye mfumo wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Tanzania imeanza kunufaika na mpango wa kuzifutia kabisa nchi maskini duniani madeni ya Taasisi za Fedha za Kimataifa kufuatia kundi la nchi nane tajiri duniani (*G8*) kukubali kufutwa kwa madeni ya nchi 22 masikini ikiwemo Tanzania. Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) tayari limeifutia Tanzania deni lake kwa Shirika hilo lenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 336. Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) pia zimetangaza kwamba zitaifutia Tanzania madeni yake kwa Mashirika hayo. Kiasi kitakachofutwa kitafahamika kwa uhakika kabla ya Julai, 2006. Aidha, Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la *Millennium Challenge Corporation (MCC)* imeiingiza Tanzania katika kundi la nchi zitakazofaidika na msaada wa *Millennium Challenge Account* na tayari tumefaulu katika awamu ya kwanza ya *Threshold* na sasa tunatayarisha mpango wa awamu ya pili *(Compact Programme)*.

Serikali iko katika hatua za mwisho za utekelezaji wa Mpango wa *PRGF* unaodhaminiwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) ambao utamaliza muda wake mwezi Desemba, 2006. Uhusiano kati ya Tanzania na *IMF* umekuwa mzuri katika miaka kumi iliyopita.

Mheshimiwa Spika, uhusiano huo umekuwa kichocheo muhimu katika kuvutia wawekezaji, kupata misamaha ya madeni na ongezeko kubwa la misaada ya wahisani ikiwemo Benki ya Dunia na kupanda kwa akiba ya fedha za kigeni. Hivi karibuni, *IMF* imeanzisha mpango mpya wa ushirikiano na nchi maskini ambazo zimeonyesha kuwa na uwezo wa kupanga na kusimamia chumi zao pasipo kuhitaji mikopo kutoka katika Shirika hilo. Serikali imeanza mchakato wa kujiunga na mpango huo ujulikanao kama *Policy Support Instrument (PSI)* mara baada ya mpango wa sasa kufikia ukomo mwezi Desemba, 2006. Kujiunga na mpango huu kutaleta manufaa ambayo ni pamoja na:-

(i) Kuvutia uwekezaji;

(ii) Gharama ndogo za usimamizi kwa kuwa kutakuwa na tathimini mbili tu kwa mwaka ikilinganishwa na ziara nyingi za maafisa wa *IMF* chini ya mpango wa *PRGF;* na

(iii) *IMF* haitatoa mikopo tena kwa Tanzania, isipokuwa kama kuna dharura, hivyo tutapunguza utegemezi kwa shirika hilo.

Misingi na shabaha ya Bajeti za mwaka 2006/2007. Kama nilivyoeleza hapo awali, Bajeti ya mwaka 2006/2007 ni ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne, kufuatia Uchaguzi wa Rais na Wabunge uliofanyika mwezi Desemba, 2005. Bajeti ya mwaka 2006/2007 imelenga kuanza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Aidha, Bajeti hii inaendeleza utekelezaji wa MKUKUTA ili kufikia malengo ya milenia na hatimaye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Kama ilivyoeleza leo asubuhi Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwekezaji, Malengo ya uchumi mpana ni pamoja na :-

(i) Pato halisi la Taifa litakua kwa asilimia 5.9 mwaka 2006, asilimia 7.3 mwaka 2007, na asilimia 7.7 mwaka 2008.

(ii) Kasi ya upandaji wa bei haitazidi asilimia 4.0 (kwa bei za mwaka 2001) ifikapo Juni 2007.

(iii) Ukusanyaji wa mapato ya ndani sawa na asilimia 14.5 ya Pato la Taifa mwaka 2006/2007, asilimia 14.7 mwaka 2007/2008 na asilimia 14.8 mwaka 2008/2009.

(iv) Ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana, ($M_2$) litauwiana na ukuaji wa uchumi, na kasi ya mfukumo wa bei.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Bajeti hii inaanza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Baadhi ya mambo yaliyoko kwenye Ilani ya Uchaguzi yanayozingatiwa katika Bajeti hii, ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Bajeti ya mwaka 2006/2007 inachochea ongezeko la kasi ya kukua kwa uchumi;

(ii) Ruzuku ya mbolea, mbegu na pembejeo za kilimo na mifugo, pamoja na miundombinu ya umwagiliaji imeongezwa katika Bajeti hii;

(iii) Bajeti imetenga fedha za kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji na uzalishaji wa bidhaa za kuuza nchi za nje *(SEZ* na *EPZ);*

(iv) Fedha zimetengwa kwa ajili ya zoezi la kutambua mipaka ya vijiji, Hati za kumiliki ardhi, ili matumizi ya ardhi yawe endelevu nchini kote;

(v) Zimetengwa fedha pia kwa ajili ya upimaji wa maeneo ya wafugaji ili kudhibiti uharibifu wa mazingira;

(vi) Serikali itaendeleza dhana ya kuunda mifuko ya udhamini wa mikopo na kuboresha uendeshaji wa mifuko ambayo tayari ipo; na

(vii) Ziko hatua nyingine nyingi katika marekebisho ya kodi ambazo nitazielezea baadaye katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi unakwenda sambamba na utekelezaji wa MKUKUTA, Dira ya Maendeleo hadi 2025 na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (*MDGs*). Kuanzia katika Bajeti ya mwaka 2005/2006, fedha kwa ajili ya utekelezaji wa MKUKUTA ziligawanywa kwa kuzingatia maeneo makuu matatu ya kimatokeo *(Outcome Clusters)*. Mwaka 2005/2006, asilimia 39 ya matumizi yote ya kutekeleza MKUKUTA zilielekezwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; asilimia 43 kwa ajili ya kuboresha maisha ya watu na ustawi wa jamii na asilimia 18 iliyobaki ilitumika kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

Katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007, maeneo yote makuu yameongezewa fedha, ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa MKUKUTA wa kuongeza rasilimali kwa ajili ya kukuza uchumi, kama msingi wa mkakati endelevu wa kuondoa umaskini.

Kwa hiyo, asilimia 45.8 ya fedha za kutekeleza MKUKUTA zitatumika kwa ajili ya kukuza uchumi. Maeneo yanayohusika ni pamoja na miundombinu, kama kuendeleza na kukamilisha miradi ya barabara na kukamilisha mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika miji ya Shinyanga na Kahama, fedha kwa ajili ya kuongeza uwezo wa *TANESCO* kuzalisha Megawati takribani 145 zaidi za umeme ili kukubaliana na upungufu wa nishati hiyo kila panapotokea ukame. Kwa ujumla, Bajeti hii imetenga asilimia 26 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ikilinganishwa na asilimia 18 zilizotengwa mwaka 2005/2006. Lengo ni kujenga mtandao mzuri wa miundombinu, ili kupunguza gharama za uzalishaji nchini na hivyo kuvutia uwekezaji zaidi kutoka ndani na nje. Tukifanikiwa katika hilo, tutaweza kuanza kusindika sehemu kubwa zaidi ya mazao yetu. Aidha, hatua za kuboresha huduma za jamii, kuboresha maisha na ustawi wa kila Mtanzania, zimetengewa asilimia 35.8 za fedha za kutekeleza MKUKUTA. Asilimia 18.4 iliyobaki imetengwa kuimarisha utawala bora.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa wananchi ni sehemu muhimu ya mpango wa kuhakikisha maisha bora kwa kila Mtanzania, kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Ili kufanikisha azma hii, Bajeti ya 2006/2007 imezingatia mambo yafuatayo:-

Kwanza, mifuko iliyoko ya dhamana za mikopo itaimarishwa ili wananchi wengi zaidi waweze kuitumia kujiletea maendeleo.

Pili, taratibu za kuanzisha Mfuko wa Dhamana kwa Mikopo ya Maendeleo zitakamishwa ili mfuko huo uanze kutoa dhamana ya mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali inaandaa taratibu ambazo zitawezesha uanzishwaji wa *SACCOS* za makundi mbalimbali ya jamii, ambayo yatawezeshwa kupata mikopo ambayo kutoka benki za kibiashara mikoani, nchini kote.

Nne, hatua za dhati zitachukuliwa kuongeza wigo wa kuzalisha umeme nchini na kuboresha mtandao wa usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, tano, fedha zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya kutengeneza vitambulisho vya Uraia ili kuwawezesha Watanzania kudhibiti maliasili yao.

Sita, kuendeleza juhudi za kuiwezesha *TIB* kutoa mikopo ya uzalishaji kwa sekta za uchumi, zikiwemo sekta za viwanda, kilimo na utalii.

Hatua ya kwanza ya kuipatia benki hiyo mtaji ni kutumia fedha za Serikali zilizokuwa zinasimamiwa na Benki hiyo mtaji kutumia fedha za Serikali zilizokuwa zinasimamiwa na benki hiyo, zisizopungua shilingi 17 bilioni. Kwa mujibu wa mizania ya vitabu vya hesabu za *TIB*, benki hiyo ina mtaji wa shilingi bilioni 7.4 unaotokana na faida ambayo benki imekuwa inapata katika miaka ya hivi karibuni. Ukiongeza shilingi bilioni 17.5 za Serikali ambazo *TIB* imeruhusiwa kuziingiza kwenye mtaji, benki hiyo sasa ina mtaji wa shilingi bilioni 24.9. Hata hivyo, ili benki hii iweze kuanza shughuli za Benki ya Maendeleo mtaji wake hauna budi uongezwe ufikie angalau shilingi bilioni 50 kwa kuanzia.

Saba, suala la mikopo ya nyumba *(Mortage Finance)*, mikopo ya mali ya kukodi yaani *lease finance*, mikopo midogo midogo yaani *Micro Finance* nalo litapewa kipaumbele katika Bajeti ya mwaka 2006. Serikali imekubaliana na wakuu wa benki zote zilizopo hapa nchini kuunda kamati maalumu ya kutafuta muafaka wa majawabu ya malalamiko kuhusu ukosefu wa mikopo, riba kubwa za mikopo na ndogo kwa amana, huduma za benki kujikita kwenye miji mikubwa tu, benki nyingi kupendelea wateja wakubwa, benki kupendelea kununua dhamana za serikali badala ya kukopesha na mengine mengi. Kamati hiyo itaundwa ndani ya mwezi mmoja na itatoa mapendekezo yake kwa serikali mwezi Oktoba 2006.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine za uwezeshaji nitazielezea chini ya marekebisho ya Mfumo wa Kodi na ada mbalimbali.

Mheashimiwa Spika, miezi michache iliyopita, Serikali ilitangaza hatua mbalimbali za kulinda mazingira ili kuweka msingi endelevu wa shughuli zetu za maendeleo. Hatua hizo ni pamoja na kupiga marufuku usafirishaji wa magogo ili kulinda misutu na vyanzo vya maji, kuondoa mifugo katika maeneo ha vyanzo vya mito na pia kupiga marufuku utengenezaji na uingizaji nchini wa mifuko myembamba ya plastiki. Bajeti ya 2006/2007 imetenga shilingi 9.4 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati wa Kutunza Mazingira.

Mheshimiwa Spika, ziko hatua nyingine kadhaa za kulinda mazingira ambazo nitazieleza baadaye kidogo.

Mheshimiwa Spika azma ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa Serikali imezingatiwa katika MKUKUTA na pia katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi. Kwa hiyo, Bajeti ya mwaka ujao wa fedha imetenga shilingi trilioni 1, milioni 4 kwa ajili ya mishahara, ikilinganishwa na shilingi bilioni 682 zilizotengwa mwaka 2005/2006, ongezeko la shilingi 318 bilioni. Fedha hizo ni kwa ajili ya nyongeza ya mishahara pamoja na ajira mpya ya walimu, watumishi wa afya, wahasibu, wakaguzi wa ndani, na wengine. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, ataelezea kwa mapana zaidi matumizi ya fedha hizo wakati atakapowasilisha bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, hii ni hatua ya mwanzo ya kurekebisha mishahara ya Serikali, mpango wa maboresho hayo ya mishahara wenye upeo na ambao ni endelevu utakamilishwa baada ya Tume ya Mishahara iliyoundwa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni kuwasilisha taarifa yake kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mapato ya Ndani. Katika mwaka 2006/2007 Serikali inalenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi trilioni 2 bilioni 460, milioni 995 (shilingi 2,460,995 milioni) sawa na asilimia 14.5 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na mapato ya shilingi trilioni 2, bilioni 66, milioni 752 (shilingi 2,066,752 milioni) mwaka 2005/2006 ambalo ni ongezeko la asilimia 19.1. Ili kuendelea kuboresha ukusanyaji, hatua zifuatazo zitatekelezwa:-

Moja, kuendelea kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipakodi wapya na kuimarisha uchumi tulivu, pamoja na kuimarisha na kuweka mazingira bora ya biashara kuwezesha sekta binafsi kukua.

Mbili, kusimamia kwa karibu mageuzi makubwa yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato *(TRA)* chini ya Mpango wake wa Pili wa Maboresho wa miaka mitano, ambao umekuwa msingi wa kukua kwa mapato ya ndani mwaka hadi mwaka.

Tatu, kuendelea kurekebisha mfumo wa kodi na kuimarisha Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa kuboresha utendaji.

Mheshimiwa Spika, nne, kuweka nguvu zaidi katika kuboresha usimamizi na utendaji wa Forodha kwa kuongeza uwajibikaji, matumizi ya teknolojia na kupunguza mlolongo wa taratibu ndefu ambazo ni kero kwa walipa kodi.

Tano, kupitia upya msingi na taratibu za misamaha ya kodi kwa lengo la kuziba mianya ya kukwepa kodi.

Sita kufanya tathmini ya makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kwa lengo la kubaini mapungufu yaliyopo na kufanya marekebisho ili kuongeza ufanisi wa kukusanya mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu misaada na mikopo ya nje, kama nilivyoeleza awali, utekelezaji wa Mkakati wa Pamoja wa Kusimamia Misaada yaani *Joint Assistance*

*Strategy* na ule wa madeni utaendelea kuisaidia Serikali kuboresha uhusiano wetu na nchi wahisani pamoja na mashirika ya fedha ya kimataifa ili tuendelee kupata misaada na mikopo yenye masharti nafuu kugharamia mipango yetu ya maendeleo. Misaada na mikopo kutoka nje itachangia takribani asilimia 39 ya Bajeti ya mwaka 2006/2007 ukiondoa misamaha ya madeni ya Mashirika ya Fedha ya Kanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi, kama nilivyosema awali, Bajeti hii inadhamiria kuanza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kwa kuzingatia vipaumbele katika maeneo yaliyoainishwa katika Ilani hiyo na katika MKUKUTA. Aidha, Serikal itaendelea kuongeza ujuzi wa watumishi wake, kuimarisha nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na kuhakikisha uwajibikaji katika ngazi zote za Serikali, zikiwamo Halmashauri za Serikali za Mitaa. Mtandao wa *IFMS* ambao umeonyeshga mafanikio makubwa katika udhibiti wa matumizi ya Serikali utasambazwa katika Halmashauri nyingi zaidi ili usaidie katika kuweka uwazi na uwajibikaji. Mtandao wa *IFMS* ni teknolojia ya mawasiliano inayozuia mtumishi kutumia fedha ambazo hakuruhusiwa, yaani ambazo hazikukasimiwa. Ni vyema Halmashauri, kupitia sheria ndogondogo, zikajipanga vizuri kusimamia fedha zinazopelekwa huko ili zitumike kama inavyokusudiwa. Waheshimiwa Wabunge mnayo nafsi ya kusaidia kusukuma jambo hili, hasa kwa kuwa ninyi pia ni Madiwani katika Halmashauri zenu.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza umuhimu wa kuchuja watumishi ili wale ambao sio waadilifu, na wanaofuja fedha za Serilai wachulikuwe hatua za kisheria. Halmashauri zinahimizwa kutoa taarifa za mapato na matumizi kila mwezi. Aidha, wananchi wanakumbushwa kuzingatia wajibu wao wa kuhoji matumizi ya Halmashauri zao kwa kufuatilia taarifa za mgao wa fedha kwa Halmashauri hizo. Kwa upande wake, Serikali Kuu itajitahidi kutoa msaada wa kila aina kuziwezesha Halmashauri kujenga uwezo wa utendaji na utaalam hasa katika fani ya uhasibu na ukaguzi wa ndani. Hivi sasa, Serikali ipo kwenye zoezi la kuajiri wahasibu na wakaguzi wa ndani kwa ajili ya Halmashauri ambao wanategemewa kuanza kazi mwezi Julai, 2006. Aidha, Wizara ya Fedha imeunda kitengo maalum cha kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika kupanga mgao wa fedha za bajeti kwa mwaka wa fedha 2006/2007, mambo yafuatayo yamezingatiwa:-

Moja, shilingi bilioni 641, milioni 766 (shilingi 641,766 milioni), sawa na asilimia 26 ya mapato yatokanyo na vianzo vya ndani, zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi bilioni 219, milioni 240, (shilingi 219,240 milioni) zimetengwa kwa ajili ya miradi maalumu ya kuzalisha umeme wa gesi katika vituo vya Ubungo na Kinyerezi, na ukarabati wa miundombinu ya kusambazia umeme.

Mheshimiwa Spika, mbili, Sekta ya kilimo pia imepewa kipaumbele kwa kiwango cha kuridhisha katika Bajeti ya 2006/2007 kwa kutambua kwamba ni sekta yenye uwezo mkubwa wa kukuza uchumi na kuongeza ajra. Bajeti ya maendeleo ya kilimo imesambaa katika Wizara nyingi - Kilimo, Chakula na Ushirika, Mifugo, TAMISEMI, Halmashauri za Wilaya, Miundombinu, na nyingine.

Tatu, Bajeti ya 2006/2007 imetenga shilingi bilioni 21 milioni 196 (shilingi 21,196 milioni) ambazo ni mgao wa asilimia 4.5 ya misaada ya nje kwa ajili ya Serilai ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) . Utaratibu wa sasa wa kugawa misaada na mapato mengine utaendelea kutumika hadi hapo utaratibu mwingine utakapopendekezwa na Tume ya Pamoja ya Fedha na kuridhiwa na Serikali zetu mbili.

Nne, Bajeti inaendelea kutenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya huduma za jamii yaani Elimu, Afya, Maji na kadhalika.

Tano, Bajeti hii imezingatia mahitaji ya msingi ya sekta zaUlinzi na Usalama wa Raia, pamoja na ufufuaji wa makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa.

Sita, Bajeti ya 2006/2007 imetenga fedha kwa ajili ya mikoa ya pembezoni na ununuzi wa magari kwa Wilaya zenye mahitaji zaidi, hasa Wilaya mpya.

Saba, mahitaji ya miradi maalum yamezingatiwa katika bajeti ya 2006/2007 kwa mfano, Mradi wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi (*Special Economic Zones)*, Mradi wa Maji Ziwa Victoria hadi Miji ya Shinyanga na Kahama; ujenzi wa barabara, na Ununuzi wa mitambo ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mfumo wa kodi, ada mbalimbali na hatua nyingine za mapato. Serikali imependekeza kuchukua hatua mpya za kurekebisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kuboresha mfumo wa kodi, kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali, kuongeza mapato ya Serikali, kuhamasisha utunzaji wa mazingira na kuweka mazingira mazuri ya uwezesjaji wa wananchi kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazopendekezwa zinahusu kurekebisha sheria za kodi zifuatazo:-

(a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, sura namba 148.

(b) Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004.

(c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, sura namba 147.

(d) Sheria ya Ushuru wa Barabara, sura namba 220.

(e) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004.

(f) Sheria ya Uwekezaji Tanzania, sura namba 38.

(g) Sheria ya Madini, sura namba 123.

(h) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, sura namba 290.

(i) Kodi ya Usimamizi wa Mafuta ya Petroli.

(j) Usimamizi wa Kodi ya Michezo ya Kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani:-

Moja, kufafanua bayana katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwamba ada ya kukodi ndege (*aircraft leasing fees*)inayolipwa na Kampuni ya Ndege iliyosajiliwa hapa nchini haitozei Kodi ya Ongezeko la Thamani, sawa na ilivyo kwa gharama ya kununua ndege. Kodi hii iliondolewa ili kupunguza gharama za uendeshaji wa kampuni za ndege nchini na hivyo kuyaongezea uwezo wa ushindani.

Mbili, kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa gesi kupitia *LPG* na mitungi ya kuhifandia gesi hiyo ili kuhamasisha wananchi kutumia gesi badala ya mkaa na kuni kwa matumizi ya nyumbani ili kulinda mazingira.

Tatu, kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kahawa inayosindikwa nchini kama ilivyo kwa chai, ili kufufua uzalishaji na mauzo ya nje ya kahawa.

Nne, kupunguza ukomo wa muda wa kuomba merejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kutoka miaka mitano hadi mitatu ili kuondoa mianya ya kukwepa kodi.

Tano, kuongeza kiwango cha adhabu ya kutotoa stakabadhi kutoka shilingi 200,000/= za sasa hadi shilingi 500,000/=.

Mheshimiwa Spika, sita, kurekebisha kiwango cha adhabu kwa kosa la kukwepa kodi kwa njia ya udanganyifu kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 2,000,000 tu ili kiwe kisichopungua shilingi 2,000,000 au mara mbili ya kodi iliyokwepwa kutegemea kipi ni kikubwa, au kifungo cha miaka miwili, au faini na kifungo kwa pamoja na saba, kurekebisha kiwango cha adhabu kwa kosa la kushindwa kulipa kodi au kushindwa kuwasilisha fomu za merejesho ya kodi kwa wakati unaotakiwa kutoka shilingi 200,000 hadi shilingi 500,000 au kiasi cha mara mbili ya kodi husika kutegemea kipi ni kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya kodi ya mapato:-

Moja, kupunguza kodi ya mapato kwa makampuni mapya yatakayojisajili katika soko la Mitaji la Dar es Salaam yaani *DSE* na kuuza angalau asilimia 35 ya hisa zao kwa wananchi ili kiwango cha kodi kiwe asilimia 25 badala ya asilimia 30 ya mapato. Punguzo hili litakuwa kwa muda wa miaka mitatu. Lengo ni kushawishi makampuni mengi ya binafsi kujiunga na soko la mitaji na kuongeza umiliki wa wananchi katika makampuni ya Tanzania.

Mbili, kutoa unafuu wa kodi ya mapato kwa watu binafsi wanaochangia mfuko wa elimu kama ilivyo hivi sasa kwa biashara. Wachangiaji watatakiwa kujaza fomu za marejesho ili kudai nafuu hii ya kodi.

Tatu, kubadilisha utaratibu wa kutoza kodi ya mapato ya hitimisho la ajira yaani *Terminal benefits,* isipokuwa pensheni ambayo haitozwi kodi ili mapato aliyolipwa mstaafu katika kipindi cha miaka sita ya mwisho au kipindi halisi cha ajira ndio yatumike kukokotoa kodi badala ya utaratibu wa sasa wa kutoza kodi mapato hayo kwa mkupuo kama mapato ya mwaka mmoja, hatua hii itapunguza sana mzigo wa kodi kwa wafanyakazi wanapostaafu.

Nne kupunguza kiwango cha kodi ya zuio, kwa mapato ya riba ya Mifuko ya Uwekezaji wa pamoja yaani *Collective Investment Schemes* kutoa asilimia 30 hadi asimilia 10 kama ilivyo kwa watu binafsi ili kuhamasisha uwekezaji wa pamoja nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa.

Moja, kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya taa, kutoka shilingi 122 kwa lita hadi shilingi 52 kwa lita ili kuhamasisha wananchi kutumia mafuta ya taa badala ya mkaa na kuni kwa matumizi ya nyumbani na hivyo kulinda mazingira. Hatua hii ya kupunguza kodi kwenye mafuta ya taa inaweza kuongeza tatizo la ukwepaji wa kodi kwa kuchnganya mafuta ya taa na mafuta mengine ya petroli yaani *fuel adulteration*. Kwa hiyo, tutahitaji kuimarisha udhibiti katika biashara ya mafuta ya petroli.

Mbili, kuongeza viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa mbalimbali zisizo za petroli kwa asilimia 7 sawa na kiwango cha sasa cha mfumko wa bei. Lengo ni kulinda thamani halisi ya mapato ya Serikali kutoka kwenye vyanzo hivi. Viwango vya sasa na vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Vinywaji baridi kutoka shilingi 41.50 kwa lita hadi shilingi 45 kwa lita.

(b) Bia inayotengenezwa kwa nafaka ambayo haijaoteshwa kutoka shilingi 150 kwa lita hadi shilingi 161 kwa lita.

(c) Bia nyingine zote kutoka shilingi 256 kwa lita hadi shilingi 274 kwa lita.

(d) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kisichozidi asilimia 25 kutoka shilingi 820 kwa lita hadi shilingi 878 kwa lita.

(e) Vinywaji vikali kutoka shilingi 1,216 kwa lita hadi shilingi 1,302 kwa lita.

(f) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo:-

(i) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 4,170 hadi shilingi 4,462 kwa sigara elfu moja.

(ii) Sigara zenye kichungi na zinazotengezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka shilingi 9,840 hadi shilingi 10,529 kwa sigara elfu moja.

(iii) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 17,870 hadi shilingi 19,195 kwa sigara elfu moja.

(iv) Tumbaku ambayo iko tayari kutengenezwa sigara yaani *cut filler* kutoka shilingi 9,025 hadi shilingi 9,657 kwa kilo.

Tatu, kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasialiano ya simu za mkononi yaani *mobile phone airtime* kutoka aslimia 5 hadi asilimia 7 ya mauzo ili kukaribiana na kiwango cha asilimia 10 kinachotozwa Uganda na Kenya wanachama wa Jumuiya ya Afirka Mashariki.

Nne, kurekebisha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ili bidhaa zinazouzwa nje ya nchi ziandikwe kwa kuuzwa nje tu au *for export only* ili kuzuia bidhaa hizo kuuzwa hapa nchini bila ya kulipa kodi.

Tano, kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa mifuko ya *plastic* inayoruhusiwa kutoka asilimia 15 hadi asilimia 120 ili kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Sita, kuweka Ushuru wa Bidhaa kwa kiwango cha asilimia 20 kwa magari madogo chakavu yenye umri wa miaka 10 au zaidi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Barabara. Ili kulinda mapato ya Mfuko wa Barabara kwa kuzingatia ongezeko la gharama za matengenezo, inapendekezwa kuongeza Ushuru wa Barabara kutoka shilingi 90/= kwa lita hadi shilingi 100/= kwa lita na kuweka kifungu katika Sheria kinachoruhusu marekebisho ya kiwango hiki kila mwaka kulingana na kiwango cha mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashiriki, kikao cha pamoja cha Mawaziri wa Fedha wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kilichofanyika tarehe 8 Juni, 2006 Mjini Arusha kilipendekeza marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Forodha kwa mwaka 2006/2007 kama ifuatavyo:-

(i) Kurudisha ushuru wa asilimia kumi kwenye mafuta ghafi ya kupikia *(Crude Palm Oil)* kwa lengo la kuwalinda wazalishaji wa mbegu za mafuta hapa Afrika Mashariki na kuziba mianya ya kukwepa kodi.

(ii) Kupunguza kiwango cha ushuru unaotozwa kwa malighafi ya kutengeneza sabuni au *(RBD Palm Stearin)* kutoka asilimia ishirini na tano hadi asilimia kumi. Lengo

ni kuwawezesha wazalishaji wadogo wa sabuni kumudu ushindani usio wa haki kutoka nje.

(iii) Kufuta Ushuru kwenye mitungi ya gesi (*LPG Cylinder*s) ili kuhamasisha matumizi ya gesi kwa nia ya kulinda mazingira.

(iv) Kupunguza ushuru kwenye karatasi zinazoagizwa kutoka nje kwa matumizi mbalimbali kama vile kuandikia na kuchapisha makala za magazeti kutoka asilimia ishirini na tano hadi asilimia kumi. Hatua hii inategemewa kupunguza gharama za uzalishaji viwandani na uchapishaji wa makala mbalimbali kama magazeti na kadhalika.

(v) Kutoa msamaha wa ushuru kwa vifaa vinavyotumia mionzi ya jua kuzalisha umeme. Hatua hii itahamasisha wananchi kutumia nishati hii mbadala na kuhifadhi mazingira.

(vi) Kuongeza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia thelathini na tano hadi asilimia hamsini kwa viberiti vinavyoagizwa kutoka nje ya Afrika Mashariki. Lengo ni kulinda kiwanda chetu cha viberiti kutokana na ushindani usio wa haki.

(vii) Kuondoa ushuru unaotozwa kwenye globu zinazohifadhi umeme. Hatua hii inategemewa kupunguza matumizi ya nishati ya umeme na gharama za umeme.

(viii) Kupunguza Ushuru viunganisho yaani *unassembled completely knocked down* vya baiskeli na pikipiki kwa waunganishaji wanaotambuliwa na mamlaka husika kuwa asilimia kumi kwa pikipiki na asilimia sifuri kwa baiskeli. Hata hivyo, pikipiki na baskeli ambazo huagizwa kutoka nje zikiwa zimekwisha unganishwa zitaendelea kutozwa ushuru wa asilimia ishirini na tano kwa pikipiki na asilimia kumi kwa baiskeli.

(ix) Kuingiza kwenye jedwali la tano la Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa msamaha kwa vifaa na madawa yanayotumika kwenye maabara kufanya uchunguzi wa magonjwa.

(x) Kuongeza Ushuru wa mazulia ya sakafuni *(floor carpets)* hadi asilimia ishirini na tano kwa kuwa hii ni bidhaa inayotengenezwa kwa kiwango cha kutosha katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(xi) Kupunguza Ushuru kutoka asilimia kumi hadi sifuri kwenye malighafi zinazotambulika katika kuzakusha karatasi yaani *HS Code 2507.00.00. HS Code 2526.10.00, HS Code 2526.20.00.*

(xii) Kupunguza Ushuru kwenye jamii ya mkaa wa mawe (*HS Code 2704.00.00)* kutoka asilimia kumi hadi sifuri ili kuendana na kiwango cha ushuru wa mkaa.

(xiii) Kupunguza ushuru kwenye malighafi itumikayo kutengeneza bidhaa mbalimbali kama vile dawa ya mswaki *(HS Code 3402.13.00)* kutoka asilimia ishirini na tano hadi asilimia kumi.

(xiv) Kupunguza ushuru kwenye malighafi zinazotumika kutengeneza vipuri vya magari (*Oil/Air/Fuel Filters - HS Code 4805.40.00)* kutoka asilimia kumi kwenda sifuri.

(xv) Kufuta Ushuru wa Malighafi inayotumika kutengeneza nyaya za kuchomelea *(welding electrodes) HS Codes 7223.00.00, HS Code 7505.11.00, 7505.12.00.*

(xvi) Kutenganisha bidhaa za kioo za *(HS Code 7019.90.00)* ili kufuta ushuru wa forodha kwenye nyuzi za kioo zinazotumika kutengeneza vifaa vya kusagia na kukata *(HS Code 7019.90.0).*

(xvii) Kutenganisha karatasi za aluminia *(HS Code 7607.19.00, 7607.20.00)* ili kutofautisha kati ya zile zilizochapishwa na zisizochapishwa. Lengo ni kuongeza ushuru kwa zile zilizochapishwa kutoka asilimia kumi hadi asilimia ishirini na tano. Marekebisho haya ya Ushuru wa Forodha yatatangazwa rasmi kwenye Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kutoza kodi sukari inayoingizwa nchini kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya *SADC* kwa viwango vinavyotozwa bnidhaa hiyo kutoka nje ya Afrika Mashariki chini ya Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika Jumuiya ya *SADC*, biashara ya sukari haipo kwenye utaratibu wa kawaida wa kupunguziana ushuru bali imewekewa utaratibu wa pkee ambapo baadhi ya nchi zimepewa viwango maalum *(quotas)* vya kuuza sukari katika soko la Afrika Kusini.

Katika utaratibu huo, Tanzania haikupewa kiwango maalum *(quota)* kwa vile haijitoshelezi mahitaji yake ya ndani. Aidha, kuruhusu sukari kuingia nchini kwa kiwango kidogo sana cha kodi (asilimia 25) kunaweza kudumaza jitihada za uzalishaji wa ndani zenye lengo la kujitosheleza kwa bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Uwekezaji ili:-

(i) Kifungu Na. 19(2) cha Sheria hiyo kinachoikataza Serikali kubadili mfumo wa kodi kwa wawekezaji kitumike kwa Wawekezaji Mahiri tu kama waliowekeza kwenye kilimo, miradi mikubwa ya kuzalisha kwa ajili ya kuuza nje, miundombinu, na mingine ya namna hiyo;

(ii) Kuondoa msamaha wa kodi unaotolewa sasa kwa magari madogo ya binafsi *(non utility vehicles)* kwa wawekezaji. Msamaha uendelee kuweko kwa magari ya kazi (*utility vehicles).*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini, inapendekezwa kutoa msamaha wa mrahaba kwa wazalishaji wa chumvi wanaotumia rasilimali zinazojirejesha *(renewable*

*resources)* ili kusaidia kampeni ya kupambana na magonjwa yanayotokana na ukosefu wa madini joto mwilini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, inapendekezwa kufuta ada ya magari yanayotumia barabara za miji *(city plying fees)* inayotozwa chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ili kuondoa kero na kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kodi na usimamizi wa mafuta ya petroli, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika eneo hili:-

(i) Kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bei ya mafuta ya petroli ili kupunguza mzigo wa ongezeko la bei za mafuta hayo, lakini bila kuathiri mapato ya Serikali. *(Makofi)*

(ii) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwa mafuta ya petroli kama ifuatavyo:-

(a) Petroli *(MSP* na *MSR)* shilingi 315 kwa lita;

(b) Dizeli *(GO)* shilingi 292 kwa lita;

(c) Mafuta ya taa *(IK)* shilingi 52 kwa lita;

(d) Mafuta mazito ya mitambo *(HFO)* shilingi 109 kwa lita;

(e) Dizeli ya kuendeshea mitambo viwandani *(IDO)* shilingi 366 kwa lita;

(f) Gesi ya kupikia ya *LPG* haina kodi; na

(g) Mafuta ya ndege *(JET A1* na *AVGas)* hayana kodi.

(iii) Kuongeza muda wa usafirishaji wa mafuta ya petroli kwenda nchi za jirani kutoka siku 15 hadi siku 30. Hatua hii itarahisisha biashara ya mafuta ya petroli bila kuathiri mapato ya Serikali.

(iv)Kuboresha utaratibu wa kurejesha kodi za Ushuru wa Bidhaa *(excise duty)* na Ushuru wa Barabara *(fuel levy)* kwenye mafuta ya petroli kwa makampuni ya madini yenye msamaha ili uzingatie uzalishaji na mauzo ya madini nje ya nchi, kulingana na uwiano uliopo kati ya matumizi ya mafuta na uzalishaji wa dhahabu. Hatua hii inalenga kudhibiti mianya ya ukwepaji wa kodi.

(v) Kuunda kikosi maalumu ndani ya Mamlaka ya Mapato kitakachosimamia utaratibu wa marejesho ya kodi kwa makampuni ya madini.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Kodi ya Michezo ya Kubahatisha, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika eneo hili:-

(i) Kuipa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Madaraka ya kukusanya kodi kutoka kwenye kianzio hiki kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato.

(ii) Kubadilisha utaratibu wa kutoza kodi ya michezo ya kubahatisha ili, badala ya utaratibu wa sasa wa kutoza viwango maalum kwa vifaa vya kuchezea michezo hiyo, kodi hiyo itozwe kwa kiwango cha asilimia 13 ya mapato yote yatokanayo na michezo ya kubahatisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda wa kodi mpya kutumika. Hatua hizi mpya za kodi zitaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2006 isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, majumuisho, kwa kuzingatia misingi na sera za Bajeti nilizoeleza hapo awali, Serikali inatarajia kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi trilioni 2, bilioni 460, milioni 995 (shilingi 2,460,995 milioni) katika mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, Serikali katika mwaka 2006/07 imepanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 4, bilioni 850, milioni 588 (shilingi 4,850,588 milioni). Kama ilivyokuwa kwa miaka kadhaa iliyopita matumizi ya Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa, yanajumuisha malipo ya kodi zote zinazotozwa kwenye bidhaa zinazotumiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo haya, sura ya Bajeti ya mwaka 2006/2007 inakuwa kama ifuatavyo:-

| | | | **Shilingi milioni** |
|---|---|---|---|
| | **Mapato** | | |
| A. | Mapato ya Ndani | Trilioni | 2,460,995 |
| B. | Mikopo, Misaada na Misamaha ya madeni ya nje | Trilioni | 2,226,116 |
| C | Kupunguza akiba *(reserve draw down)* | Bilioni | 163,477 |
| **Jumla ya Mapato ya Ndani na Nje** | | **Trilioni** | **4,850,588** |
| D. | Matumizi ya Kawaida | Trilioni | 3,116,121 |
| | (i) Deni la Taifa | Bilioni | 287,786 |
| | (ii) Wizara | Trilioni | 2,087,536 |
| | (iii) Mikoa | Bilioni | 60,554 |
| | (iv) Halmashauri | Bilioni | 730,285 |
| E. | Matumizi ya Maendeleo | Trilioni | 1,734,467 |

(a) Fedha za Ndani Bilioni 641,776
(b) Fedha za Nje Trilioni 1,092,701

**Jumla ya matumizi trilioni 4, 850,588.**

Mheshimiwa Spika, mwisho, Serikali ya Awamu ya Nne imejipanga kutekeleza kwa dhati Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inasisitiza kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi na ajira ili kupunguza umaskini, hasa wa kipato. Bajeti ya 2006/2007 pia ni mwendelezo wa jitihada za Serikali katika kufikia malengo ya MKUKUTA, malengo ya milenia na hatimaye Dira ya Maendeleo 2025.

Hata hivyo, ili kufikia lengo letu mapema zaidi, kila mwananchi anapaswa kushiriki kikamilifu kwa kutumia fursa zinazojitokeza kwa kuzalisha mali na kujiongezea vipato. Ni vizuri ieleweke kwamba Serikali haitoi fedha kwa mwananchi mmoja mmoja katika kupiga vita umaskini, bali jukumu la Serikali ni kuboresha mazingira yatakayowezesha wananchi kuongeza uzalishaji, ajira na kujiletea maisha bora. Serikali iko tayari kutimiza wajibu wake huo.

Mheshimiwa Spika, ushiriki katika uzalishaji kwa mwananchi mmoja mmoja au katika vikundi ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wetu. Aidha, sekta ya viwanda ikiboreshwa na kutilia mkazo usindikaji wa mazao ya kilimo, ina nafasi kubwa ya kuchangia Pato la Taifa na kukuza ajira. Bajeti hii pia inalenga kuendeleza jitihada za Serikali za kuunganisha nchi yetu kwa njia ya miundombinu ya barabara, reli, mawasiliano na nishati. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge wataniunga mkono katika Bajeti hii inayolenga kufikia matumaini ya wananchi wetu waliotuchagua.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:**Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Kama tulivyokubaliana na kama ulivyo utamaduni wa Bunge letu, baada ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha anayewasilisha Bajeti huwa tunaahirisha Bunge hadi Jumatatu ya wiki inayofuata.

Kabla sijatoa matangazo mengine, naomba niwatambue wawakilishi muhimu baadhi yao wakiwa wanawakilisha nchi ambazo zimechangia hii bajeti yetu ambao wako hapa nasi leo. Naomba niwatambulishe Mheshimiwa Balozi wa Uholanzi *(The Netherlands)* tunaomba asimame, *the Ambassador of Netherlands please, His Excellency the Ambassador of the United State of America, the Representative of the International Monetory Fund, the Country Representative of the International Labour Organization. We also have represented here by the following friendly countries with*

*whom we do well considerable trading, his Excellency the Ambassador of Zimbabwe, his Excellency the Ambassador of Angola, his Excellency the Ambassador of Mozambique and His Excellency the Ambassador of Indonesia. These are the only ones I have been notified although I see quite gathering in the gallery, I can't speculate so I will just stop there*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Fedha na Uchumi Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, anaomba Kamati ikutane kesho saa 3.30 asubuhi ghorofa ya pili. Nadhani pale ghorofa ya pili mkifika hapo mtaelekezwa chumba kinachostahili.

Kuhusu utaratibu wetu tayari nimepata wachangiaji Waheshimiwa Wabunge 75. Lakini tukumbuke pia kwamba kabla ya wao kuchangia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi atawasilisha maoni ya Kamati na amepewa muda wa saa moja.

Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani Waziri Kivuli wa Fedha, ambaye pia ndiyo Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed amepewa nusu saa siyo kwamba Upinzani umeonewa, walivyojipanga wao atakayezungumzia mambo ya fedha ni Waziri mmoja na Waziri Kivuli wa Uchumi Mheshimiwa Kabwe Zitto, ameniarifu yeye eti atawasilisha Mpango wa Uchumi Mbadala. Kwa hiyo, naye kapewa nusu saa. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, upande wa Kamati ya Fedha na Uchumi ni saa moja na upande wa Kambi ya Upinzani ni saa moja. Kwa hiyo, ni sahihi tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumamosi kuna semina kuhusu mapambano yanayoendelea dhidi ya gonjwa la UKIMWI, Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa na kila kitu kimeandaliwa kama ilivyo desturi katika ukumbi wa Bunge wa zamani. Mwenyekiti ni Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MBUNGE FULANI:** Saa ngapi?

**SPIKA:** Jumamosi tarehe 17 Juni, 2006 saa 4.00 asubuhi katika ukumbi wa zamani wa Bunge.

Baada ya matangazo hayo, nataka niwatakie Waheshimiwa Wabunge *weekend* njema na sasa natangaza kuliahirisha Bunge hadi siku ya Jumatatu, tarehe 19 Juni, 2006 katika ukumbi wetu huu saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.13 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu tarehe 19 Juni, 2006 saa tatu asubuhi)*